# TOLEO LA PILI LA MPANGO KAZI WA USULUHISHI WA AKIIRA GEOTHERMAL LIMITED.

AkiiraGeothermalLimited 36 Njia ya Muiri, Karen Nairobi S.L.P 15546–00509 Langata Nambari ya Simu: +254 712 196 549 Barua pepe: info@akiiraone.com Tovuti: http://www.akiiraone.com/

# YALIYOMO


| SURA | Maelezo | Ukurasa |
|---|---|---|
| **1** | **USULI NA MUKTADHA** | **1-4** |
| | 1.1 Kusudi na Malengo | 1-4 |
| | 1.2 Muktadha wa eneo na usuli wa kihistoria | 1-4 |
| | 1.3 Muktadha wa mradi na mabadiliko ya mienendo | 1-6 |
| | 1.4 Historia ya Mpango Kazi wa Usuluhishi | 1-7 |
| | 1.5 Mazingatio na Mapungufu | 1-8 |
| **2** | **MFUMO WA SHERIA** | **2-1** |
| | 2.1 Mfumo wa Kisheria wa Kenya | 2-1 |
| | 2.2 Haki za Kibinadamu za Kimataifa na viwango vya EIB | 2-2 |
| **3** | **MAPUNGUFU KATIKA MCHAKATO UNAOHITAJI SULUHISHO** | **3-1** |
| | 3.1 Hatua iliyopelekea kufukuzwa kwa lazima | 3-1 |
| | 3.2 Mapungufu dhidi ya sheria za Kenya na Viwango bora vya utendaji | 3-1 |
| **4** | **ATHARI NA USULUHISHI WA KUSTAHIKI** | **4-1** |
| | 4.1 Athari za kufukuzwa | 4-1 |
| | 4.1.1 Historia ya kufukuzwa na athari zinazoathiri Lorripil | 4-1 |
| | 4.1.2 Historia ya, na athari zinazoathiri MlimaTatu | 4-1 |
| | 4.2 Kustahiki na Haki | 4-2 |
| | 4.2.1 Vigezo vya kustahiki | 4-2 |
| | 4.2.2 Mbinu za uamuzi wa kustahiki | 4-2 |
| | 4.2.3 Vigezo vya Kustahiki vya Lorropil | 4-2 |
| | 4.2.4 Mantiki (sababu) ya kina za kustahiki katika Lorropil | 4-2 |
| | 4.2 5 MlimaTatu- Kustahiki na Haki ya Kurebisha | 4-4 |
| | 4.2.6 Sababu za Kina za kustahiki katika MlimaTatu | 4-4 |
| **5** | **MBINU ZA USULIHISHAJI** | **5-1** |
| | 5.1 Mpango wa Ushiriki wa Wadau | 5-1 |
| | 5.2 Utaratibu wa kutatua malalamishi | 5-1 |
| | 5.2.1 Muhtasri wa utaratibu wa malalamishi ya AGL | 5-1 |
| | 5.2.2 Daraja la kwanza: Ngazi ya jamii | 5-1 |
| | 5.2.3 Daraja la Pili :Ngazi ya Baina ya Jamii mbili au zaidi | 5-2 |
| | 5.2.4 Daraja la Tatu: Kamati ya malalamishi ya Kaunti ndogo | 5-2 |
| | 5.2.5 Kukata Rufaa kwa Azimio | 5-2 |
| | 5.3 Uainishaji wa Waathiriwa | 5-3 |
| | 5.3. 1Kitengo cha kwanza- Jamii yaLorropil– Waathiriwa 13 | 5-3 |
| | 5.3 2 Kitengo cha Pili -MlimaTatu– Waathiriwa 14 | 5-3 |
| | 5.3.3 Kitengo cha Tatu- Jamii ya Lorropil– Waathiriwa 31 | 5-3 |

5.4 Mchakato wa Usuluhishaji 2022 5-3
5.4.1 Ushirikiano wa Jamii 5-4
5.4.2 Ushirikiano wa kibinafsi na Waathiriwa 5-4
5.4. 3 Gharama ya Jumla ya Usuluhishi 2022 5-5

5.5 Malalamishi yanayotokana na malipo ya Usuluhishi 5-5

5.5.1 Mkutano wa kwanza wa daraja la kwanza; Oktoba 25,2022 katika afisi ya AGL, Naivasha 5-6
5.5.2 Mkutano wa pili wa daraja la kwanza ; Desemba 8,2022 katika afisi ya AGL,Naivasha 5-7
5.5.3 Mkutano wa kwanza, daraja la tatu, Mei 11, 2023 katika Shamba la Boffar ,Naivasha 5-7
5.5.4 Mkutano wa pili, daraja la tatu ,Mei 18, 2023 katika Shamba la Boffar , Naivasha 5-8
5.5.5 Mkutano wa tatu, daraja la tatu,Juni 15,2023 katika shamba la Boffar ,Naivasha 5-8
5.5.6 Mkutano wa nne, daraja la tatu, Septemba 22,2023, katika Hoteli Montana, Naivasha 5-8
5.5.7 Mkutano wa ufuatiliaji wa daraja la tatu, Oktoba 12, 2023, katika Hoteli Montana,Naivasha 5-8

5.6 Awamu ya pili ya malipo ya upatanishi 2023 5-9

5.7 Jumla ya Waathiriwa na gharama ya malipo ya usuluhishi hadi sasa. 5.9

5.8 Jumla ya Waathiriwa na gharama ya usuluhishi ambao hujalipwa hadi sasa 5-9

5.9 Bajeti ya kero zisizotarajiwa za utatuzi 5-10

**6 UFUATILIAJI, UWAJIBIKAJI NA CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA WAATHIRIWA 6-1**

6.1 Maoni ya ufuatiliaji wa Waathiriwa yatasasishwa, Machi 2024 6-1

6.2 Wajibu wa utekelezaji 6-2

6.3 Changamoto za utekelezaji 6-2

6.4 Hitimisho 6-3

# ORODHA YA YALIYOMO


| Sura | Maelezo | Ukurasa |
|---|---|---|
| Jedwali 3-1: | Muhtasari wa Mapungufu dhidi ya mchakato unaotazamiwa kisheria na viwango vya kimataifa katika kufukuzwa kwa lazima | 3-1 |
| Jedwali 4-1: | Vigezo vya kustahiki | 4-2 |
| Jedwali 4-2: | Haki ya Lorropil kupata suluhu | 4-3 |
| Jedwali 4-3 | Haki ya MlimaTatu kupata Suluhu | 4-4 |
| Jedwali 4-4: | Vigezo vya kustahiki na na vya kupeana alama na mifumo ya haki | 4-1 |
| Jedwali 5-1: | Gharama ya jumla ya malipo ya usuluhishi mwaka wa 2022 | 5-5 |
| Jedwali 5-2: | Malalamishi yalipokelewa ju ya malipo ya Usuluhishaji | 5-5 |
| Jedwali 5-3: | Jumla ya gharama ya malipo ya Usuluhishaji | 5-9 |
| Jedwali 5-4: | Jumla ya Malipo ya Usuhuluhishi ambayo hayajalipwa hadi sasa | 5-9 |
| Jedwali 6-1: | Muhtasari wa Ufuatiliaji wa Waathiriwa | 6-1 |

# 1 USULI NA MUKTADHA

## 1.1 Madhumuni na Malengo

Makala haya ni toleo lililosasishwa na Mpango Kazi wa Usuluhishi.(RemAP-2)
Usasishaji huo umetokana na uhitaji wa mchakato wa kutatua malalamishi uliotokea tangu kuchapishwa kwa ripoti ya awali mnamo Novemba 2022 na unaonyesha hali ya sasa ya juhudi ya usuluhishi, hadi mwisho wa Februari 2024.
.
Inakusudiwa kusomwa kwa kushirikiana na mfumo wa kwanza wa sera ya Uhamisho wa Julai 2022 na Mpango Kazi wa Mwisho wa Usuluhishi [1] wa 2022, ambayo hapo awali uliundwa kama mfumo wa hali ya juu wa kutambua kustahiki na stahili za wahusika walioathiriwa na kuongoza hatua zitakazo ongozwa na AGL ili kutoa suluhu kuhusiana na athari zinazohusiana na mchakato na kufukuzwa mnamo Novemba 2019.
Ripoti hii si mpango kamili wa utekelezaji wa makazi mapya kulingana na Viwango ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) au Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na haijumulishi habari za kina za fidia, au hatua za utekelezaji, bajeti au mahitaji ya rasilimali kulingana na muda uliyowekwa.

## 1.2 Muktadha wa eneo na usuli wa kihistoria

Kampuni ya Akiira 1 Geothermal Ltd (AGL) inapatikana mkabala na kusini mwa eneo la makazi ya RapLand yenye watu waliohamishwa kutokana na shughuli za joto ardhi zilizopakana nayo upande wa kaskazini na magharibi.
RapLand ni eneo la karibu ambalo linatoa huduma za umma kama vile usambazaji wa maji, elimu, afya na utawala za serikali za mitaa kwa jamii jirani ambazo bado wanaishi nje ya maeneo ya jotoardhi.
Kwa hivyo huvutia watu kutumia raslimali za RapLand wanapozihitaji.

Kinyume na matakwa ya wakaazi wa RapLand, uzio uliwekwa kaskazini na kusini mwa eneo ya makazi ya Kampuni ya kuzalisha umeme ya Kenya (KenGen) hivyo kuzuia kupita kwa wanyama nje ya ua.
Kwa kuweka uzio huo, KenGen imeifungia RapLand hiyvo kumaanisha wafugaji wa kimaasai wanaweza tu kupata malisho katika eneo la Kedong kwa kuvuka kupitia ardhi ya AGL.
Uzio unazunguka eneo la AGL pande zote isipokuwa upande wa kaskazini ambapo Ranchi ya Kedong ipo.
Katika Ranchi ya Kedong kuliishi vikundi mbalimbali ya wafanyakazi wa zamani na famlilia zao na washirika. Ili kujikimu kimaisha, wanajishughulisha na uchomaji wa makaa, kazi za kawaida na ufugaji. Wafugaji wa ngombe hasa ni Wamaasai lakini wafugaji wa mbuzi na kondoo wanatoka katika makabila mbalimbali ambayo kihistoria wamekuwa wakulima na wafugaji na hivi karibuni wanajishughulisha na njia mbalimbali za kujikimu kimaisha kama vile uchomaji makaa, biashara ndogondogo na ajira.

Eneo la Mradi wa AGL limetumiwa na wenyeji katika ufugaji na uchomaji makaa katika kipindi cha miaka minane iliyopita hivyo shinikizo la kupata maeneo mapya ya ardhi limeongezeka na wametafuta malisho na miti ya makaa katika nyanda za juu za Olkaria.
Pia waliingia na kutumia mali asili ndani na karibu na eneo la Mradi wa AGL.
Kama inavyoweza kuonekana kwa kupitia upya mifumo ya ukazi a makazi ya muda yalijengwa na kukaliwa kwa miaka kadhaa hadi rasilimali katika kila eneo zilipokwisha.
Uvamizi na makazi kwenye ardhi ya AGL ulifanyika katika maeneo mawili; moja Mlima Tatu, magharibi mwa ardhi ya AGL, na mwingine katika eneo linalojulikana kama Lorropil kaskazini mwa eneo, mkabala na makazi ya RapLand.

[1]https://frontier.dk/akiira-geothermal-project/
[2]Na KenGen.

Jamii isiyokuwa ya Kimaasai ambao waliishi na kuendeleza utafutaji wa riziki katika eneo la Ranchi ya Kedong na mashamba ya AGL, hawakuwa wakaazi wa kudumu lakini walihama kutoka sehemu moja hadi nyingine kutafuta miti ya kuchoma makaa. Viongozi wa Kitrukana wa jamii ya Kambi, walitambua kuwa jamii yao, walihama na kuishi katika makaazi yao ya sasa(Ranchi ya Kedong) baada ya ya Wamasaai kupewa makazi mapya katika shamba la Rap. Kulingana na hawa viongozi na jamii ya Mlima Tatu, makazi ya kwanza ya kudumu yaliyoundwa kwenye ardhi ya AGL yalikuwa Mlima Tatu. Makazi ya Mlima Tatu, yanajulikana kienyeji kama Ndonyoni au Lorengelup ( katika lugha ya Turkana, hii ina maana ya mahali penye mchanga mwekundu, na walowezi wanaweza kuwa walianzisha aina fulani ya uwepo wa kudumu katika eneo lile.

Makazi ya Lorropil yaliundwa baada makazi ya Mlima Tatu kuundwa na walowezi wa kwanza walikuwa wanaume ambao walihusika katika uchomaji makaa.Jamaa za jumuiya zote mbili walijenga nyumba zilizo wima na zilizojengwa kwa vijiti vya mbao na karatasi za nailoni. Miundo hii ilijengwa baada ya jamii ya Wamaasai kuhamishwa katika ardhi ya Rap. Kutokana na hali ya uhamaji wa jamii hizi mbeleni, walijenga nyumba za muda zilizotengenezwa kwa karatasi za nailoni ambazo zingeinuliwa juu ya mapengo kwenye vichaka na ingetoa makaazi ya usiku kucha au hata mvua inaponyesha.

Kuna dhana miongoni mwa jamii za Wamaasai kwamba kuwepo kwa jamii zisizo za Wamaasai wanaoishi katika Ranchi ya Kedong na karibu na AGL, kunaleta ushindani wa raslimali na fursa zinazoweza kupatikana kwa makampuni ya Jotoardhi katika eneo hilo. Kwa mfano; kazi, mipango ya uwajibikaji kwa jamii na kadhalika. Fauka ya hayo, kuzidisha mivutano iliyopo katika eneo la mradi, Ranchi ya Kedong imependekeza kuwapa makazi jamii ya Kambi Turkana kwenye sehemu ardhi iliyo karibu na Pedi 2 ya AGL. Hii ina maana kuwa, shughuli zozote za siku za usoni ambazo AGL itataka kufanya katika Pedi 2, basi italazimika kuzingatia jamii zisizo za Wamaasai ambao watakuwa jirani wa karibu. Shughuli hizi zinaweza kujumuisha utambuzi wa hatari na athari mpya za Mazingira na Kijamii ambazo zinaweza kuathiri jamii ya Kambi Turkana.

.

## 1.3 Muktadha wa mradi na mabadiliko ya mienendo

AGL ilichimba visima viwili vya uchunguzi kwenye eneo lake la ekari 1,000 mwaka wa 2015. Wafanyakazi wenye ujuzi wa mpango huu wa kuchimba visima walitoka sehemu mbalimbali za Kenya. Wakati wa awamu ya kabla ya kuchimba visima, AGL iliajiri watoa huduma wa usalama wa ndani. Pia iliajiri kampuni mbili za Maafisa wa Uhusiano wa Jamii (CLO) zinazopatikana nchini ambazo tangu 2014, wamewakilisha kampuni kwa majirani zake katika ardhi ya Rap na Kusini karibu na Kambi Turkana huko Kedong/ Ranchi ya Akiira. Wao, pamoja na wafanya kazi wa usalama, wamekuwa kiolesura cha kampuni na jumuiya hata wakati ambapo hakuna shughuli za uchunguzi za kuchimba visima.

Eneo la AGL lilinunuliwa kutoka kwa Ranchi ya Kedong ambaye ni mmiliki na meneja wa Ranchi za Kedong na Akiira. Ranchi ya Kedong imeuza sehemu za ardhi yake kwa ajili ya nishati ya joto ardhi, vifaa na maendeleo mengine ya viwanda. Hali hii ya Kedong kuuza ardhi zaidi ambayo haitumiki kibiashara huenda ikaendelea. Ardhi ya Kedong, pamoja na eneo lililonunuliwa na AGL, ilikuwa mojawapo ya madai ya Masaai wa Suswa kwamba, kihistoria ardhi ilikuwa yao. Walitaja umiliki usio wa halali, lakini hilo lilifutiliwa mbali mahakamani mwaka wa 2014.

Mpango wa Utekelezaji wa Wadau wa 2015 wa AGL ulizingatia muktadha huu nyeti. Ulizingatia mipango ya ushirikiano wa washikadau wa makampuni mengine ya jotoardhi na kubainisha jumuiya zake zilizoathirika kuwa 'zile ambazo zinaweza kuathiriwa na maendeleo ya jotoardhi. Athari hizo ni pamoja na sulfidi hidrojeni, kelele, utitiri wa magari na watu. Jamii nyingi zilizoathirika kutokana na Mpango wa Utekelezaji [3], zitakuwa ndani ya umbali wa kilomita tano kutoka eneo la mradi wa Akiira 1 Geothermal Company Limited.

Suswa pia ilijumuishwa kama jumuiya kuu ya wadau iliyo nje ya eneo la athari. Kamati nne za jumuiya zilizotambuliwa kama wawakilishi wa watu walioathirika na Mradi ziliwajumulisha Wamasaai pekee kwa madhumuni ya ushirikishwaji. Hii ilitokana na uelewa wa AGL juu ya utata wa mahusiano ya Wamaasai na makundi mengine yasiyo ya Wamaasai katika eneo hilo na pia madai yao ya awali ya kihistoria ya eneo hilo.

Kabla ya 2019, RapLand wala Akiira hawakuwa na nyua na matumizi ya raslimali na huduma zingine ulikuwa wazi. Jamii ya Wamasaai bado inashikilia mtazamo wao wa upekee wa haki za kutambuliwa na uhalali kuhusu haki ya kihistoria na harasa iliyotokana na kupoteza kwa mashamba yao, rasilimali, kikwazo kikiwa uwepo wa wasio Wamaasai, pamoja na kampuni zote zilipo hivi sasa za Jotoardhi.

Picha za satelaiti za eneo katika ardhi ya AGL iitwayo Lorropil, kwenye mpaka wa Rapland zinaonyesha kuwa makazi hayo yalianza kama maeneo yaliyokuwa karibu na Rapland na kwenye ardhi ya Kedong/AGL yaliondolewa wakati wa ujenzi wa Rapland. Utitiri wa watu kwenye ardhi ya AGL ulifanyika wakati wa kampeni ya 2019 ya kuchimba visima.

Mnano Julai 2019, ekari elfu nne za Ranchi ya Kedong zilitunukiwa Kitet-Sossion Masaai katika suluhu ya nje ya mahakama ya Kedong. Ingawa inaokena hadharani kama utambuzi wa haki za watu wa eneo hilo, bado inadaiwa ardhi hii imechukulia na Wamasaai wasio wenyeji, hivyo kuongeza kuwaudhi wenyeji.

[3]AnnexV.AkiiraGeothermal Limited Mpango kazi ya Wadau, katika AkiiraGeothermal Limited(AGL)Tathmini ya Athari za Kimazingira na kijamii kwa Kiwanda cha Nguvu cha Joto Ardhi cha Akiira, katika Kaunti ndogo ya Naivasha, Kaunti ya Nakuru, Rasimu ya Mwisho na ERM,Mei 2016.
4 Tazama Mapungufu ya Sheria ya Matendo Kipengele Cha 22 ya Sheria ya Kenya , Sehemu ya 13, kwa madai ya umiliki mbaya.
5 Ikiwa ni pamoja na Ombi Nambari 57 ya 2014 ,Mahakama Kuu ya Kenya, Nakuru (Parkire Stephen Munkasio & wengine 14 wanaoishi kwenye ardhi yenye nambari ya marejeleo,8396 (i.r 11977) huko Kedong) v Kedong Ranch Limited & wengine 8 [2015] eKLR) waliodai bila mafanikio 'umiliki halali wa ardhi hiyo kwa madai kuwa ni ardhi ya mababu zao na ardhi ya jamii'…(wao) 'wamepata hati miliki ya ardhi kwa kumiliki kinyume cha sheria au kwa maagizo'.

Maafisa wa serikali wa eneo na kaunti waliripotiwa kuwarejelea makundi mseto ya wakaazi wa Akiira/ Ranchi wa Kedong kama 'maskwota. Kudai haki za maskwota na kuondoa ulimiliki usio wa halali [4] katika eneo hili umefanywa tu na vikundi vya Wamasaai kwa kutumia sheria ili kudhibitisha ufikiaji wa haki zao za mababu katika ardhi ya Kedong kwa zaidi ya miaka kumi [5]. Madai hayo yametolewa tu na Wamaasai pekee.

Wavamizi wa ardhi wa mradi wa Akira huko Lorropil na mawakili wao walipendekeza kwa Naibu kamishna wa Kaunti [DCC] kwamba walikuwa na haki ya kufidiwa. Kulingana na shuhuda huru kutoka kwa msemaji wa jamii ya Turkana, wakili wao, wavamizi wenyewe na Wamaasai wa Rapland, wavamizi wa Lorropil na Mlima Tatu wanaokataa kutoka shamba la AGL na kufukuzwa mwaka wa 2019 , walikuwa na lengo la kulipwa fidia.

Ili kupata fidia, wawakilishi wao wa umma, waliojiteuwa( msemaji na wakili wa jamii ya Turkana ) walijaribu kuonyesha ya kwamba, wameishi ' kwa muda mrefu katika eneo hilo. Kwa kifupi, ilidokeza hadhi yao kama maskwota. Masimulizi kutoka kwa vikundi vya Wamasaai wa Rapland na Suswa yameendelea kukashifu madai haya kwa vile wanayaona kuwa haramu na yenye ushindani. Ili kuimarisha haki za maskwota, jamii katika eneo hilo zimeanzisha vikundi vya ustawi kisheria ambavyo vimetambuliwa na maafisa wa serikali ya maeneo.

## 1.4 Usuli wa mpango wa Usuluhishi

AGL imerekodi ushirikiano wake na walowezi katika eneo la Lorropil tangu uchimbaji wa visima uanze mwaka wa 2016.Katika mikutano yote ya robo mwaka iliyorekodiwa na jumuiya kwanzia Novemba 2016, na kuendelea, AGL iliwashauri wawakilishi wa walowezi hao kwamba wanapaswa kuhama na kwamba hawakuwa na haki ya kulipwa fidia. Mnamo Aprili 2019, AGL ilitoa ombi maalum kwa mwakilishi aliyejiteua wa Lorropil kukomesha wimbi la wavamizi na kumhoji kuhusu usaidizi wake unaoshukiwa kuwezesha kufurika kwa wavamizi.Mkutano wa ufuatiliaji mnamo Mei 2019 na wawakilishi wa Lorropil ulidhibitisha tuhuma za AGL na kutoka wakati huo hadi siku ya ziara ya DCC huko Lorropil mnamo tarehe 22 Juni 2019 kutoa notisi ya usemi ili waondoke ama wafurushwe, AGL ilikuwepo kwenye mkutano wa timu ya usalama na usimamizi wa Kedong ilikujadili kuhusu wavamizi na kupanga, arifa yao ya kuondoka.

Marekebisho zaidi yamefanywa kwenye toleo hili kufwatia mchakato wa kutatua malalamiko na ushirikiano na washikadau wakati wa utekelezaji wa toleo la kwanza la ripoti wa mpango kazi wa usuluhishi.

Mara AGL ilipomaliza kusafirisha [6] ekari 1000 za ardhi, tarehe 10 Septemba,2019 ilitoa ombi rasmi [7] kwa serikali kuwaondoa watu ambao walikuwa wamevamia ardhi yake.

Amri ya pili ya kufukuzwa iliyopitishwa kwa usemi tarehe 12 Septemba, iliripotiwa kwenye vyombo vya habari na ilisemekana kutolewa na DCC ofisini kwake.

Notisi ya mwisho ilitolewa katika makazi yao tarehe 28, Oktoba 2019 ikitoa ilani ya wiki moja ya kuondoka.Ufurushaji ulitekelezwa na polisi chini ya maagizo kutoka kwa timu ya usalama ya kaunti ndogo.

Baadhi ya makazi yalichomwa moto tarehe 3 na 4 Novemba 2019. Wiki mbili baadaye, miundo katika eneo la Mlima Tatu iliteketezwa. Polisi kutoka Mai Mahiu waliripoti kwamba wavamizi Wakikuyu kutoka Mai Mahiu walikuwa miongoni mwa waliofurushwa kutoka Lorropil.

Katika jitihada za kupata maoni ya wadau wa jamii wa eneo hilo, kulikuwepo na kikao katika ofisi ya AGL mwishoni wa mwezi wa Januari 2020 na kikao hicho kuhudhuriwa na wawakilishi watano kutoka Suswa na pia wawakilishi sita kutoka jamii ya RapLand. Baada ya mkutano, walitangaza kuwa kutakuwepo na 'msaada mpana wa jamii' kwa Mradi.

Baada ya kufukuzwa, ofisi ya chifu eneo la RapLand iliweza kuwahifadhi waathiriwa waliofukuzwa kutoka eneo la Lorropil na hawakuwa na pengine pa kwenda. Pia walikubaliwa kukifanya kiwanja cha ofisi ya chifu ambayo bado haikuwa inatumika na ilikuwa mkabala na makazi ya Lorripol kama makazi ya muda. Tume ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu ya Kenya (KNCHR) na Shirika la Msalaba Mwekundu, zilidhibitisha kuwa waliwafanyia waathiriwa mahojiano katika ofisi ya chifu huko RapLand. Watu wengi waliofukuzwa kutoka Lorrropil, takriban familia 35, inashukiwa kuwa walitoka eneo la MaiMahiu. Ni takriban kilomita thelathini na tano kutoka mji wa Naivasha.

Vifurushi vya misaada ya kibinadamu [8] vilitolewa na Shirika la Msalaba Mwekundu kwa takriban familia thelathini.

[6] Mnamo Agosti 22, 2019.

7Ombi hilo linataja maombi ya awali ya msaada yaliyotolewa kwa serikali za mitaa na kutembelea eneo lakini hii haikurekodiwa kama amri rasmi ya kufurushwa.

[8] Shirika la Msalaba Mwekundu lilitoa blanketi mbili, seti moja ya jikoni, mikeka miwili ,turubai mbili,vipande mbili ya sabunina na chandarua moja.

Kwa usemi,Shirika la Msalaba Mwekundu lilithibitishia Mshauri wakati wa mahojiano kwamba, takriban familia 26 hazikupokea usaidizi kwa sababu vifurushi ambavyo vilikuwa vimetayarishwa na Shirika hilo havikutosha kuwahudumia watu wote waliodai kufurushwa kutoka Lorropil. Wakiwa na au bila vifurushi vya misaada ya kibinadamu kutoka kwa Shirika Msalaba Mwekundu, watu waliokuwa wamefukuzwa kutoka Lorropil, waliondoka na kurudi kwenye makao yao ya asili au maeneo ya makaazi kama vile Rapland, Kambi ya Turkana au karibu na Naivasha.

Watu waliokuwa wakiishi Mlima Tatu, upande wa la AGL, waliondoa vitu vyao kabla ya kufukuzwa, na baadaye wengi wakayajenga tena makazi yao nje ya mpaka wa kusini wa AGL.

Ripoti hii ya sasa, ndio Mpango Kazi wa Usuluhishi kwa waliofukuzwa kutoka eneo la mradi wa Akiira 1 ya AGL

## 1.5 Mazingatio na Mapungufu

.

Mchakato wa kuunda Mpango wa hatua ya awali ya Usuluhishi(RemAP-1) ulihusisha ziara mbalimbali za mfululizo kati ya Agosti – Desemba 2020, Mei-julai 2021 na Aprili- Juni 2022 ambazo zilitokana na mabadiliko ya wigo wa kazi.

Aidha, taarifa zaidi zilipokuwa zikitolewa kwa washauri kuhusu hali ya orodha ya watu wanaotarajiwa kuathiriwa na mradi, hasa waliokuwa na makazi ya kudumu nje ya Ranchi kubwa ya Kedong iliwekwa wazi, tathmini zaidi zikiwemo, pamoja na mahojiano na waathiriwa ambao waliwekwa katika kambi za wakimbizi wa ndani za serikali pale Mai Mahiu walihitajika kuamua ufikiaji wa Usuluhishi.Maendeleo ya Mpango kazi wa Usuluhishaji (RemAP-2) ni matokeo ya mikutano kadhaa ya utatuzi wa malalamiko ambayo yamefanyika tangu 2022.

Mabadiliko makuu yaliyotokana na tathmini zaidi zilizofanywa na mshauri na yamekuwa ni uboreshaji wa vigezo vya kustahiki na mabadiliko ya hatua za usuluhishaji zinazohitajika kuhusisha waathiriwa wote wanaostahiki. Kutokana na ziara hizo za mfululizo, idadi ya waathiriwa wanaosthiki iliongezeka na kujumulisha wadai wapya watano kutoka Mlima Tatu.

Mapendekezo ya fidia katika Mpango kazi wa Usuluhishaji (RemAP-2) yalitokana na mfumuko wa bei uliodhaniwa na kushuka kwa dhamani ya dola wakati wamakubaliano lakini haya yanaweza badilika.

Kiasi kipya cha fidia kilitumika kwa wale ambao hawakuwa wamelipwa katika awamu ya kwanza ya fidia.

# 2. MFUMO WA SHERIA

## 2.1 Mfumo wa Kisheria wa Kenya

Majukumu ya haki za binadamu ya Kenya yamewekwa katika Katiba ya Kenya.Mswada wa haki, sura ya nne ya katiba, inahakikisha idadi ya haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni, na hizi zinaakisi viwango vya haki za binadamu vilivyoainishwa katika sheria za kimataifa za haki za binadamu. Kifungu cha 20 cha Katiba kinaonyesha kuwa sheria Mswada wa haki unatumika kwa sheria zote na unafunga vyombo vyote vya serikali na watu wote (pamoja na makampuni ya biashara). Kifungu cha 22 hutoa ufikiaji wa suluhu kwa mtu yeyote anayedai kwamba haki au uhuru za kimsingi katika Mswada wa Haki umenyimwa, umekiukwa au kutishiwa.

Katiba inahakikisha haki ya kumiliki mali chini ya kifungu cha 40 na sheria inaamuru kwamba, Serikali haiwezi kumnyima kiholela mtu mali yake (kifungu cha 40 (3)). Kifungu cha 40 (4) kinaonyesha kuwa masharti yanaweza kufanywa kuwalipia wakaaji fidia ya ardhi kwa nia njema, ambao wanaweza kuwa wamenyanganywa mali yao baada ya kutwaa ardhi, hata kama wakaaji hawana hati miliki ya ardhi hiyo. Kifungu cha 43(1)(b) kinasema kwamba, ‘ kila mtu ana haki ya kupata makazi ya kutosha na viwango vya kuridhisha vya usafi wa mazingira’.

Masharti mahususi yametolewa kuhusu haki za mazingira na ardhi ambayo yamefafanuliwa katika Sura ya Tano. Katiba inaainisha aina tatu za ardhi; ardhi ya umma ambayo inatawaliwa na kifungu cha 62, ardhi ya jamii ambayo masharti yake yamehakikishwa katika kifungu cha 63 na ardhi ya kibinafsi ambayo imeandikwa katika kifungu cha 64. Ili kutekeleza masharti ya Sura ya Tano, Bunge limetunga sheria zinazohusiana na ardhi kama vile Sheria ya Ardhi, 2012 na marekebisho ya mwaka 2016; Sheria ya Usajili wa Ardhi, 2012; Sheria ya Ardhi ya Jamii, 2016; na Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Ardhi, 2012

Taratibu za uondoaji zimerekebishwa katika Sheria za Ardhi (Marekebisho) ya mwaka 2016 na kanuni za mwaka 2017. Kufukuzwa ni halali iwapo kutafuata taratibu hizi. Taratibu halali za kufukuzwa zinatoa rufaa kwa watu walioarifiwa kwa mahakama kusitisha kufukuzwa. Ikiwa tu sababu itapatikana kuwa ni ‘udhalimu wa kihistoria wa ardhi’, suluhu itapendekezwa. Uamuzi wa mahakama unategemea uhalali wa utaratibu wa arifa inayotekelezwa, pamoja na madai. Mahakama inaweza kulinda wahusika dhidi ya kufukuzwa kwa lazima.

Sera ya Ardhi ya Kenya inatetea jukumu la serikali katika kuhesabu maskwota wote, kujadili na kuwezesha kuhalalisha makazi au uhamishaji upya na dhamana ya umiliki kama inavyofaa. Maskwota wana haki ya umiliki wa ardhi baada ya kukaa katika ardhi hiyo, bila usumbufu na kuendelea kukaa kwa muda wa miaka 12 tangu wakati mmiliki aliyesajiliwa anapopata habari kuhusu uvamizi huo. Wanaweza kutoa madai ya kisheria ya umiliki kulingana na 'umiliki mbaya' wa ardhi wanayomiliki.

Sheria ya Uvukaji Mipaka (L.N.1964, Rev 2012) inatoa ruhusa kwa mmiliki au polisi kuwakamata wavamizi wa mashamba bila kibali lakini wanapaswa kwenda kwa hakimu mara tu wanapokamatwa. Mahakama inaweza kumtia ndani mhalifu na kumuamuru kuondoka ndani ya kipindi maalum kilichowekwa. Kutofuata agizo, mahakama itaidhinisha mtawala au afisa wa polisi kumuondoa mtu huyo pamoja na mali yake [9].

Mwezi wa Septemba mwaka wa 2021, Kenya ilikuwa taifa la kwanza Barani Afrika kuandaa mpango wa Kazi wa Kitaifa kuhusu Biashara na Haki za kibinadamu (BHR NAP) 2020- 2025. Mpango wa kazi wa Kitaifa uliidhinishwa rasmi na Bunge la Kitaifa na likatoa mfumo wa udhabiti kwa BHR. Kwa mujibu wa Kanuni Elekezi za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Kibinadamu(UNGPs). Mpango wa Kazi wa Kenya( NAP), umeainisha vipaumbele vya sera za kitaifa kwenye BHR kwa kuzingatia vipengele tano: 1. Ardhi na mali asili, 2. Uwazi wa mapato, 3. Ulinzi wa mazingira, 4. Kazi na 5. Upatikanaji wa suluhu.

Pia ina hatua za kisera kwa kila moja ya mihimili mitatu ya Kanuni za Umoja wa Kimataifa ambazo ni: (i) Wajibu wa Serikali wa Kulinda Haki za Kibinadamu, ii) Wajibu wa Shirika ni

Kuheshimu Haki za Kibinadamu na iii) Upatikanaji wa suluhisho. Upatikanaji wa suluhu Madhubuti umesisitizwa kwani iligundulika kuwa biashara nchini Kenya huwa hazitambui shughuli hatari zinazoathiri haki za kibinadamu na kuzipunguza au kuziepuka. Ikiwa madhara yangetokea, hawakuweza kuhakikisha kuwa waathiriwa wanapata suluhu madhubuti - ikiwa serikali ilikuwa inalinda haki zao za kibinadamu. Mpango wa Kazi wa Taifa, unapendekeza ahadi za sera za haki za binadamu, utimilifu wa uzingatiaji wa haki za binadamu, kuripoti, na ushirikiano na washikadau husika ili kuwezesha suluhisho ya ukiukaji wa haki za binadamu unaohusiana na biashara. Unajumuisha dhamira muhimu zaidi ya Serikali ya kuelekea kitaifa kufuata viwango hivi vya kimataifa vya haki za binadamu.

9Kwa hivyo wakati mmiliki wa ardhi ya kibinafsi apowaagiza mara kwa mara wakaaji waliopo hapo  kinyume cha sheria kuondoka na hawafanyi hivyo, mmliki anaweza:1. Kuwashtaki mahakamani kama wavunja sheria, ambapo adhabu na ufurushwaji unawezakuhitajika ukaombwa na kuamrishwa; au 2 Kutumia stakabadhi rasmi (Form LA.57) wape notisi ya kuondoka ya moja kwa moja kati ya muda wa miezi tatu, baada ya muda huo, hatua itakayofuata ya kuwaondoa itakuwa kufurushwa kwa mmujibu wa taratibu za kisheria.

## 2.2 Haki za Kimataifa za Binadamu na viwango vya EIB

Utendaji mzuri wa kimataifa, Katiba na sheria ya Kenya inalinda dhidi ya kufukuzwa kutoka kwa makazi mapya na inatoa hitaji la kuepuka na pale ambapo kuepukwa hakuwezekani inahakikisha haki ya kupata suluhu kama ifuatavyo:

Serikali ya Kenya inahitajika kulinda haki na uhuru wa raia wake kupitia kwa kuidhinisha njia za kisheria kuathiri haki hizi[10] kwa kuzingatia ukweli kwamba imeziridhia:

- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (ICESCR) – hii inasimamia haki ya kuwa na kiwango bora cha maisha ikiwa ni pamoja na chakula cha kutosha, mavazi na makazi (kifungu cha 11), haki ya afya (Kifungu cha 12), elimu (Kifungu cha 13) na kazi (Kifungu cha 6.1),
- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) – ambayo inasimamia haki ya kupata suluhisho (vifungu 2.3 na 26), na
- Mkataba wa Kikanda wa Afrika wa Haki za Binadamu; na
- Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Ulinzi na Msaada wa Wakimbizi wa ndani barani Afrika (Mkataba wa Kampala).

Kifungu cha 2 (5) na (6) cha Katiba pia hutoa msingi wa kutambuliwa kwa sheria za kimataifa kama sehemu ya sheria za Kenya. Hii ina maana kwamba viwango vya kimataifa vya haki za binadamu ambavyo vimeidhinishwa na Serikali ni sehemu ya sheria nchini Kenya na Mahakama inaweza kutumia sheria hizi za kimataifa wakati wa kutoa hukumu mahakamani.

Kwa msingi huu,wakati wa kutathmini ufurushaji, mahitaji ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (ICESCR) (Kifungu cha 11.1); Mkataba wa haki za mtoto (Kifungu.27.3), na Mkataba wa Kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake kifungu cha 14.2(h), zinatumika.

Maoni ya jumla ya nambari 711 ambayo ni tafsiri ya haki ya makazi ya kutosha kama ilivyohakikishwa katika kifungu cha 11 (1) cha ICESCR na kupitishwa na Kamati ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (CESCR), inafafanua kwamba, matumizi ya istilahi 'kufukuzwa kwa lazima' kunalenga kuwasilisha maana ya uholela na uharamu[12], na inasema kwamba pale ambapo kufukuzwa kunafanyika ikizingatiwa kuwa ni kwa haki, Mataifa lazima yahakikishe kwamba yanaweka ulinzi wote  na mahitaji yote ya mchakato unaotazamiwa[13].

[10] Utaratibu wa Haki za Binadamu za Ukanda kama vile Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa kuzingatia vifungu 14, 16 na 18 (1) vya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu Na Watu na Miongozo ya Utekelezaji wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni   katika mkataba wa Afrika ya Haki ya Binadamu umelaani ufurushaji wa lazima-Kwa mfano, angalia Kituo cha utekelezaji wa Haki za Kijamii na Kiuchumi dhidi ya Nigeria,  nambari ya mawasiliano155/96, Uamuzi wa Mei 2002.

[12] Maoni ya Jumla nambari 7 inafafanua ufurushwaji wa lazima kama ‘kuondolewa kwa kudumu au kwa muda dhidi ya matakwa ya watu binafsi, familia na / au jamii kutoka kwa maboma na/ au ardhi wanayokalia bila utoaji ,na ufikiaji wa  fomu zinazofaa za kisheria au ulinzi mwingine.’

Hii ni pamoja na haki ya kupata suluhu na mifumo ya mahakama au uwajibikaji, ikijumuisha mbinu za kupinga sababu za kufukuzwa kwa lazima. Maoni ya kijumla ya nambari 7 yanasema kwamba kufukuzwa hakufai kusababisha ukosefu wa makazi au kuwafanya watu waliofukuzwa wawe katika hatari ya kukiuka haki zingine za binadamu. Serikali inatakiwa kuchukua hatua zote ambazo zinafaa ili kuhakikisha makazi mbadala, makazi mapya, au kupatikana kwa ardhi iliyo na tija.

Kanuni na Miongozo ya Msingi ya Umoja wa Mataifa juu ya Ufukuzwaji na Uhamisho unaotokana na Maendeleo (A/HRC/4/18) inawasilisha athari za haki za binadamu za uondoaji unaohusishwa na maendeleo na inatoa miongozo inayoendana na haki ya jinsi ya kutekeleza kufukuzwa. Mwongozo hutoa mahitaji ya ufichuzi wa awali wa mipango ya kufukuzwa, fursa za kupata ushauri wa kisheria, kiufundi, na ushauri mwingine kwa watu walioathiriwa na usikilizaji wa umma unaotoa nafasi kwa watu walioathirika kupinga uamuzi wa kufukuzwa na/au kuwasilisha mapendekezo mbadala na kueleza madai yao. na vipaumbele vya maendeleo.

Ili kurekebisha ukiukaji wa haki za binadamu, kanuni na Miongozo ya Msingi ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki ya Kupata suluhu na fidia kwa wahasiriwa wa ukiukaji mkubwa wa sheria ya Kimataifa ya Haki za Kibinadamu na Ukiukaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu[14] inatofautisha aina tano za ulipaji wa fidia.

- ***Urejeshaji:*** *humrejesha aliyeathirika katika hali ya awali kabla ya ukiukaji kutokea. Vilivile hujumuisha kurejashwa kwa uhuru, kufurahia utambukisho na uraia*
- ***Ukarabati:*** *hujumuisha matibabu na huduma za kisaikolojia.*
- ***Fidia:*** *hutoa pesa kwa uharibifu uliotokea.*
- ***Uridhika:*** *inajumuisha matamshi rasmi ya kurejesha utu na sifa, msamaha wa umma, ukumbusho na heshima*
- ***Dhamana ya kutorudia:*** *inajumuisha hatua za kimuundo ambazo zitazuia kutokea tena ukiukaji kutokea.*

Kifungu cha 8 cha Tamko la Kimataifa la Haki za Kibinadamu (UDHR) na Kanuni na Miongozo ya Msingi ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki ya kupata suluhu na kulipa wahasiriwa wa ukiukaji wa sheria ya Kimataifa ya Haki za Kibinadamu na ukiukaji mkubwa wa sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, kinasema kwamba suluhisho sahihi kwa kufukuzwa kwa lazima ni kuweka wahasiriwa karibu iwezekanavyo na hali ilivyo.

Kiwango cha 6 cha Mfumo wa Uendelevu wa Mazingira na Kijamii wa EIB unaongozwa na suala la kufukuzwa kwa lazima na Tume ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Kibinadamu, kufukuzwa kwa lazima, 10 Machi 1993, E/CN.4/RES/1993/77. Inakuza matumizi ya ulinzi wa kiutaratibu wa kimataifa dhidi ya kufukuzwa kwa lazima kama ilivyoainishwa katika Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (CESCR), Maoni ya jumla ya nambari 7: Haki ya makazi ya kutosha (Kifungu.11.1): kufukuzwa kwa lazima, Mei 20. 1997, E/1998/22, na Kanuni na Miongozo ya Msingi ya Umoja wa Mataifa ya Ufukuzwaji na Uhamisho wa Msingi wa Maendeleo.

Viwango hivi pia vinasisitizwa katika Kiwango cha 5 cha Utendaji cha IFC ambacho kinahimiza kutofukuzwa kwa lazima na ikiwa uhamisho wa lazima, kufurushwa kutoka kwa makazi/ardhi kutokea na upotevu unaohusiana na riziki hauepukiki, basi ulinzi wa haki na maslahi ya watu walioathirika unapaswa kujumuishwa katika mpango wa makazi mapya au mpango wa kurejesha riziki unaokidhi viwango vya IFC.

[13]Maombi yaJumla Nambari 7 Haki ya Makazi ya Kutosha(kifungu 11(1) ya Agano): Ufurushwaji wa lazima, aya za 3 na 9..
[14] Azimio la 2005/35(UNDoc.No.E/CN.4/RES/2005/35(2005))na Azimio la GA,60/147(UNDoc.No. A/RES/60/147 (2006)

# 3. MAPUNGUFU KATIKA MCHAKATO UNAOHITAJI SULUHISHO

## 3.1 Hatua iliyopelekea kufukuzwa kwa lazima

Mchakato huu haukukidhii matakwa ya sheria ya Kenya au hata utendaji mzuri wa kimataifa kwa njia kadhaa na hivyo kuzingatiwa kuwa mchakato wa Kufukuzwa kwa Kulazimishwa. Baadhi ya njia hizo ni:

- *Ushiriki wa wadau wa kiubaguzi.*
- *Kutopeana notisi ilioandikwa kabla ya kufukuzwa.*
- *Kutoanzisha wala kutekeleza kesi ya kukiuka sheria za kisheria*
- *Ukosefu wa nafasi ya kukata rufaa*
- *Kutolinda haki ya watoto ya kupata elimu baada ya kufukuzwa*
- *Kushindwa kulinda mali ya waathiriwa kwa kukosekana kwa njia mbadala zilizotolewa au kupangwa ili kukidhi haki za watu hawa za makazi, utu afya, usalama na elimu.*
- *Ukosefu wa hatua mwafaka za kufuatwa baada ya kufukuzwa*

## Mapungufu dhidi ya sheria za Kenya na viwango Bora vya Utendaji

Mapungufu dhidi ya sheria ya Kenya au viwango vya kimataifa kutokana na hatua hizi zinazochochea haki ya kurekebisha yamefafanuliwa hapa chini na kufupishwa katika jedwali

**Jedwali3-1:Mukhtasari wa mapungufu dhidi ya taratibu zinazofaa kisheria na viwango vya kimataifa katika kufukuzwa kwa lazima**

| Haki za kibinadamu na mchakato wa kisheria ambao hukufuatwa na AGL | Haki za kurekebisha | Hatua zinazokubalika na sheria za kimataifa |
|---|---|---|
| **Ushiriki wa wadau wa kiubaguzi** | Kujumuishwa katika ushirikiano wa wadau na kupata manufaa sawia kutoka kwa mradi | Kurekebisha na kusasisha mpango wa Ushirikiano wa Wadau na baadaye kuandaa mpango kazi jumuishi. |
| **Utoaji wa notisi kamilifu ilioandikwa kabla ya kufukuza.** | Uweleo wa pamoja wa majukumu na wajibu katika sekta ya kibinafsi na ya umma | Kuunda mfumo wa sera ya makazi mapya yenye mwongozo wa kuepuka, majukumu na wajibu. |
| **Fursa ya rufaa ya kutofukuzwa** | Kuwafahamisha zaidi kuhusu haki na wajibu | Kuunda mfumo wa sera ya makazi mapya yenye mwongozo wa kuepuka |
| **Uharubifu wa makazi na upotezaji wa mali ya kibinafsi kwa kiwango kidogo wakati wakufukuzwa.** | Kufidia kwa hasara ya kibinafsi kwa thamani ya uingizwaji | Kuhakikisha kulipia hasara kwa kutumia fedha ili kuhakikisha thamani ya uingizwaji. |
| **Kupoteza ulinzi dhidi ya kufukuzwa (hadhi, afya, salama na ukosefu wa usalama)** | Kuepuka kurudia uhamisho wa lazima | Kuunda mfumo wa sera ya makazi mapya yenye mwongozo wa kuepuka. |

| | | |
|---|---|---|
| | Kukuza ulinzi ya maslahi ya wanawake na watoto wao. | Kuunda na kutekeleza mpango kazi wa Usuluhishi. |
| **Kupoteza fursa ya kupata elimu kwa sababu ya athari** | Kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata elimu | Kufuatilia na kudhibitisha kuwa wanafunzi wote wanaweza kufikia shule |
| **Ukosefu wa hatua mwafaka baada ya kufukuzwa** | Kukidhi mahitaji ya waliofukuzwa, shughuli za kujikimu kimaisha, na athari zingine zinazorekebishwa kwa uendelevu, usalama wa eneo na umiliki. | Kutathmini hali na muundo wa fidia na vifurushi vya kurejesha kurejesha riziki vinavyolingana na hasara<br><br>Kuunda na kutekeleza mpango kazi wa kurekebisha |

# 4. ATHARI NA USULUHISHAJI WA KUSTAHIKI

## 4.1 Athari za ufurushaji

Sehemu ifuatayo inaeleza historia na pia kutoa ufafanuzi kuhusu athari za mchakato wa kufukuzwa ambazo zimetambuliwa kupitia ushirikiano na walioathirika katika kila eneo.

Makala haya si mpango wa Utekelezaji wa Makazi mapya. Kwa hivyo hakuna utafiti wa kijamii na kiuchumi wa ngazi ya kifamilia na tathmini ya msingi au ya shughuli za kujipa riziki iliyowezekana ndani ya upeo mdogo wa kazi hii. Kwa hivyo athari ya kufukuzwa hazijapimika wala kuelezwa kwa kina kwa kila familia.

Tathmini ya athari/ mahitaji imetokana na ripoti ya usemi, ushirikishwaji na mwingiliano ya washika dau, pamoja na uchunguzi uliofanywa na mtaalamu wa maswala ya kijamii alipokuwa kwenye eneo na pia Mfumo wa Sera ya Uhamishaji .

### 4.1.1 Historia ya kufukuzwa na athari zinazoathiri Lorropil

Ingawa famila zote zilipata kufukuzwa, hasara zao zilitofautiana kidogo na ukubwa wa familia zao, vianzo vya riziki, makazi ya sasa na ajira zilichangia katika: (a). kubainisha aina ya suluhu zinazohitajika) na (b) aina za chaguo la malipo yanayotosheleza stahili.

Kati ya familia 31 zilizohama wakati wa utitiri, pia kufukuzwa kutoka Lorropil lakini ambao tayari walikuwa na; (a)makao ya msingi katika eneo lingine wakati wa uhamisho, na (b) wamekuwa katika eneo la Lorropil mwaka wa 2019 pekee. Inadhaniwa kwamba wengi wangesumbuliwa na kufukuzwa kutokana swala la unyonge uliowakumba, na fursa zilizopotea katika vituo vyao ya nyumbani ambazo walikuwa wameziacha kwa hiari na pia kutokana na hitaji la kulipia kurudi kwao.

.

.

### 4.1.2 Historia ya na athari zinazoathiri Mlima Tatu.

Mlima Tatu uliathiriwa na ufurushaji mara mbili ambao ulitekelezwa mwaka wa 2019. Ufurushaji wa kwanza ulifanywa na maafisa wa Huduma ya Msitu ya Kenya(KFS) na walinzi walioajiriwa na Kedong mnamo Agosti 2019. Katika ufurshaji huu wa kwanza nyumba arobaini na nane za Mlima Tatu ambazo zilikuwa kwenye ardhii ya Kedong na AGL ziliathirika. Baada ya kufukuzwa walowezi wa Mlima Tatu, walijenga mpya nyumba zao katika eneo hilo hilo. Wakati wakufurushwa kwa mara ya pili nyumba za Mlima Tatu ziliteketezwa na maafisa wa Huduma ya Kitaifa ya Polisi(NPS) waliotoka katika Kituo cha Polisi cha Kongoni mnamo Novemba. Katika ufurushaji huu wa pili, nyumba zilizoteketezwa ni zile za ardhi ya AGL tu.

Kwa familia 18 zilizotambuliwa kuwa zinastahili kulipwa fidia, nne zilihamia kutoka Mlima Tatu baada ya tukio la pili la ufurushaji na kuhamia Kambi Turkana.

Familia 14 hazikuhama kutoka eneo la Akiira-upande wa Mlima Tatu, badala yake zilijenga nyumba zao katika eneo sawia la upande wa Akiira. Hii ilikuwa mara ya pili kwa walowezi hao kujenga upya nyumba katika eneo sawia. Baada ya kujenga tena mara ya pili kwenye ardhi ya Akiira msimamizi wa usalama ya AGL alienda na kuzungumza na walowezi na kuwataka wahamie ardhi ya Kedong , jambo ambalo walifanya. Walowezi kumi na moja walihamia Ardhi ya Kedong. Kati ya familia hizi kumi na moja, nne zina makazi ya kudumu katika Kambi ya Gavana.

Wakati wa ufurushaji wa Novemba 2019, maafisa wa Huduma ya Kitaifa ya Polisi, walianza mchakato wa kuchoma nyumba huko Lorropil ambayo iko katika sehemu ya juu kuliko Mlima Tatu. Walowezi wa mlima Tatu waliweza kuona nyumba zilizokuwa zinachomwa na

wakatahadharishwa kwa polisi wangeenda pia kuchoma makazi yao baada ya kuchoma nyumba katika eneo la Lorropil. Wakazi hao walikuwa wamehamisha mali zao nje ya nyuma zao kabla ya kufurushwa, na kwa hivyo polisi walichoma miundo za nyumba hizo tu.

Kati ya familia 14 zilizoathiriwa, 6 zinaongozwa na wanawake. Kati ya familia hizo, familia moja ambayo ilikuwa na mwanamke mmoja kama kiongozi wa familia na ambaye alikuwa mtoto wa miaka miwili wakati wakufurushwa, mtoto huyo sasa ana miaka minne na kwa sasa yuko shule ya chekechea.Familia moja iliyo katika mazingira magumu yenye unyonge ilitambuliwa- wanandoa ambao wamo katika umri wa miaka 80 hawawezi kufanya kazi.

Kati ya familia kumi na nne, 6 zinaweza kuwa tayari kuondoka Kedong ikiwa zitapewa fursa bora zaidi nje ya eneo hili. Wanandoa hawa wazee ambao wamo katika miaka yao ya 80 wanaweza kutokuwa tayari kuondoka Kedong. Hii inaweza kuwa kwa sababu walikuwa wametoka kaunti ya Turkana na waliondoka sehemu hio zaidi ya miaka 60 bila kurejea. Kwa sababu hii, sehemu pekee wanahisi wanaweza kuiita nyumbani ni Kedong. Familia hio nyingine inaongozwa na mwanamke aliye na watoto wazima na watoto hawa wamehama kutoka Kedong. Mwanamke huyo ana fursa ya kuondoka katika eneo hili lakini bado hajafanya hivyo. Huenda ikawa hataki kuondoka Kedong.

## 4.2 Kustahiki na haki

Sehemu hii inaelezea vigezo vya kustahiki vilivyopendekezwa na ambavyo viliundwa baada ya kuzuru eneo la mradi mnamo 2021 na 2022 na pia utambuzi wa walioathiriwa na ushufurushaji uliotokea mnamo 2019.

### 4.2.1 Vigezo vya kustahiki

**Jedwali 4-1: Vigezo vya kustahiki**

| Sababu ya Kustahiki | Vigezo |
|---|---|
| **1** | Tarehe ya mwisho na kipindi cha kuishi(zaidi ya mwaka mmoja hadi mitano inaonyesha kudumu) huku tarehe ya kusitishwa ikiwa Juni 2019, wakati notisi ya kwanza ya kuondoka ya usemi huku tarehe ya kusitiishwaq ikiwa ni tarehe 22 Juni 2019, wakati notisi ya ya usemi ya kuondoka ilitoleea na DCC na majina ya watu walioathirika huko Lorripil yalinakiliwa<br>Kwa watu wa Mlima Tatu serikali haikuwatambua watu walioathirika na siku iliyopangwa ya ufurushaji ni tarehe 17 Novemba 2019. |
| **2** | Makazi yaliyoharibiwa wakati wa uhamisho. |
| **3** | Waliokuwepo wakati wa ufurushaji mnamo Novemba 2019 |
| **4** | Udhibitishi wa mashahidi (angalau mashahidi wawili) na kuwepo kwenye makazi wakati wa vipindi maalum vya kuishi pale na matukio ya ufurshaji pamoja na ushahidi uliowazi wa dhuluma kwa mfano makazi yaliochomwa, shuhuda zinazolingana, na kwa baadhi,ushahidi wa udhibitisho wa kudumu mahali pengine. |
| **5** | Wakaazi wakudumu pekee wa Waathiriwa ndio wapo kwenye eneo la ufurushaji. |

**4.2.2 Mtindo wa uamuzi ya ustahiki**

Mtindo wa kuunda vigezo na kuamua kustahiki ni kama ifuatavyo:

- *Uchunguzi wa mtu binafsi ulifanywa na mshauri ilikubaini waayhiriwa waliofukuzwa kwa nguvu. Utaratibu huu ulihitaji ushirikishwaji na uhakiki wa mchakato unaopelekea na kufuatizia kufukuzwa.*

.

- *Vigezo vitano vya kustahiki kwa haki ya kurekebishwa au kufidiwa viliandaliwa (4.2.1)).*
- *Kustahiki kulizingatiwa kwa kwa kufikia vigezo vyote au angalau vine kati ya vitano vilivyo ainishwa. Vigezo1,2,4 na 5 vinatumika kwa wote.kigezo cha 3 hakitumiwi kwa wakazi wa Mlima Tatu ambao walitelekeza nyumba zao na kuchkua vitu vyao kabla ya kikosi cha kufurusha kufika kwenye eneo; na,*
- *Wadai wote wametathminiwa kustahiki kwao kwa kupewa aina tofauti za suluhu kulingana na vigezo hivi.*
- *Ambapo kuna shaka kuhusu ustahiki, AGL itafuatilia na kudhibitisha.*

Mara tu ustahiki utakapobainishwa, aina mahususi na mgao wa Usuluhishi wa kila mwathiriwa unafaa kujadiliwa kulingana na hali ya mtu ya kabla ya kufukuzwa.

Katika baadhi ya matukio, hii inaweza kumaanisha kuwa ni kifurushi kamili kinacholenga kuhakikisha makazi, usalama wa umiliki kama inavyotakiwa na Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Kijamii ya Frontier[15] na kukatisha tamaa ya waathiriwa kurudi kwenye ardhi ya AGL na pia kuchagua njia bora za kujitafutia riziki.

Aidha, kwa watu ambao walifurushwa lakini walikuwa wamekuja kwenye eneo katika robo ya pili ya 2019 kudai fidia ya uongo, angalau usaidizi wa kifedha unafaa kutolewa ili kugharamikia kurudi kwa makazi yao na kufidia kwa kupoteza heshima na makazi kwa muda uliotokana na kufurushwa kwa lazima..

### 4.2.3 Vigezo vya kustahiki vya Lorropil

Walowezi asilia wa Loropill zilikuwa familia 13, ilivyodhibitishwa kutoka kwa mahojiano kwa wakazi na majirani. Katika robo ya pili ya 2019, hii idadi iliongezeka hadi familia 49.Mwakilishi wa serikali ya kitaifa alifanya sensa mnamo Juni, 23, 2019 na kubaini kuwa watu 44 ni wakazi wa Lorropil.Kupitia mahojiano na wakazi wa Kambi Turkana, mshauri kuwa watu watano ambao hawakuonekana kwenye orodha hivyo kufanya jumla ya idadi kufikia 49[1].

Wengi wa wakazi wapya kutoka eneo la Lorropil walikuwa wakimbizi wa zamani wa ndani wenye makazi ya kudumu huko Mai Mahiu (Kambi ya Gavana) na walikuwa wamepokea fidia kutoka kwa Serikali. Hawa wakimbizi wa zamani wa ndani walihamia Lorropil baada ya kuripotiwa kuvutiwa na ahadi za kulipwa fidia na mkuu aliyejiteua wa kijiji cha Lorropil, na polisi wa zamani kutoka Kongoni. Kikundi hiki na baadhi ya walowezi wa asili waliripotiwa kuunda kikundi cha kujisaidia ambacho kisajiliwa na Serikali na ada ya usajili iliripotiwa kukusanywa na mkuu wa kijiji wa Lorropil aliyejiteua.Mshauri aliamua kuwa ukusanyaji wa ada hii ya wanachama haukua na kinyume na sheria

Kulingana na swala la haki la urekebishaji, kati ya jumla ya watu 49 waliodaiwa kufukuzwa kutoka Lorropil,44 walidhibitishwa kufukuzwa, 17 wakiwa wanawake na 27 wakiwa wanaume. Watano waliojumuishwa katika orodha hiyo hawakuathiriwa na ufurushaji uliotekelezwa.

**Jedwali4-2:Vigezo vya kustahiki vya LorropilLorropil**

| Watu binafsi wanaoishi Lorropil kabla ya 2019 | Wanaumme | Wanawake |
|---|---|---|
| **13** | 9 | 4 |
| **Idadi ya watu walioingia** | Male | Female |
| **31** | 18 | 13 |
| **Idadi ya watu wasio na haki ya kupata urekebishaji kwa kufukuzwa** | | |
| **Waliotoka kabla ya kufurushwa** | Wenye hawjawahi ishi Lorropil | |
| **4** | 1 | |

### 4.2.4 Sababu za kina za Kustahiki katika Lorropil

Jumla ya watu 31 waliripotiwa kufika kwenye eneo hilo kutokana na ushawishi wa mkuu wa kijiji cha Lorropil aliyejiteua kwa matarajio kuwa wangelipwa fidia na AGL.

Aliungwa mkono na kiongozi wa kike mwishoni mwa 2018 kutoka Mai Mahiu. Wakati wa ziara zilizofuata zilizofanywa na mshauri mnamo Machi na Aprili 2022 huko Mai Mahiu na kutokana mazungumzo na Maafisa wa Serikali ya Kitaifa,mshauri aliarifiwa kwamba waliofukuzwa kutoka Lorropil walitoka katika Kambi ya Gavana [16]. Makazi haya ni takriban kilomita tano kutoka mji wa Mai Mahiu.

Kulingana na maafisa wa serikali, wakaazi wa Kambi ya Gavana ni wakimbizi wa zamani wa ndani kwa ndani wanaojishughulisha na uchomaji makaa na shughuli za kilimo katika Ranchi ya Kedong. Mshauri alifahamishwa kuwa wakimbizi wazamani wa ndani kwa ndani ni wale waliopewa makazi katika eneo hilo baada mapigano ya kikabla ya 1992, 1997 na 2007 yaliyotokea katika Bonde la Ufa.

[15]Frontier'sESMS inakubaliana na viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa ikiwa ni pamoja na PS 5 na uhitaji wa ufuatiliaji baada ya ufurushaji kuhakikisha kuwa watu wamehamishiwa na kupewa uhakikisho wa umiliki na ufufuzi wa shughuli zao za kujipatia riziki.

Mshauri huyo pia alipokea taarifa kutoka kwa maafisa wa serikali kuwa makaazi matatu katika Ranchi ya Kedong yaani: Kambi Turkana , Mlima Tatu na Lorropil yalianzisha vikundi ya kujisaidia na nia ya kutambuliwa na serikali kama maskwota kwenye ardhi ya Akiira (Mlima Tatu na Lorropil) au kwenye Kedong (Kambi Turkana). Katika mahojiano na uongozi wa Kambi Turkana, iliripotiwa kuwa wanachama wa vikundi vya kujisaidia wanatakiwa kulipa ada ya kujisajili ambayo hutumiwa na viongozi wa vikundi hivyo kuwezesha usafiri wao kuelekea ofisi mbalimbali ya serikali kutafuta msaada.

Baada ya mikutano ya awali ambapo maslahi yao yalijadiliwa, viongozi hao wawili wenye ushawishi walikwepa mikutano iliyofuata ili kuzungumzia juu ya haki zao.Mshauri alifahamishwa kuwa familia 31 zote zilitoka katika Kambi ya Gavana hata hivyo hakuna mashirikiano yaliyowezekana wakati wa ziara zilizofanywa Machi na Aprili 2022.

Kwa upande ya walowezi wa awali wafanyabiashara wawili ambao mara kwa mara waliuza bidhaa huko Lorropil ambao na walikuwa wametambuliwa kwenye orodha ya DCC ya watu waliofukuzwa, walidhibitishwa kuishi RapLand na Gichagi (kijiji karibu na Suswa kwenye Ranchi ya Kedong) mtawalia, si Lorropil.Wafanyabiashara hao wawili waliondolewa kwenye orodha ya watu wanaostahiki. Mbali na wanya biashara hao mtu ambaye alihama kutoka Lorropil kabla ya kufukuzwa pia aliondolewa. Alisema kuwa alihusika katika ugombvi na majirani zake wa Lorropil. Ugomvi ambao ulisababisha yake kuchomwa na baadaye alilipiza kisasi kwa kuchoma nyumba zote za makazi hayo mapema (2019).
Baada ya kutoelewana huko na majirani zake, alihama Lorropil na hakuathiriwa na ufurushaji wa Novemba 2019 kwa sababu alikuwa ameondoka kweye makazi hayo na alikuwa akiishi kwingine.

Kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali 4-2, jumla ya idadi ya familia zinazostahili ni 13.

***Upataji wa haki ya usuluhishi kwa ukamilifu au sehemu yake tu.***

- *Kati ya familia zinazoishi Lorropil kabla ya 2019 na zinazostahiki kupata haki ya utatuzi ni 13 tu zingestahiki kulipwa fidia kamili.*
- *Familia zote 31 za utitiri zitakuwa na haki ya kufidiwa tu sehemu ya fidia kutokana na kuwa na makazi ya kudumu nje ya Kedong*

### 4.2.5 MlimaTatu- Ustahiki na Haki ya Usuluhishi

Kati ya familia 18, ni nne tu zilihama kutoka kwa ardhi ya AGL baada ya kufurushwa na Huduma ya Misitu ya Kenya na kwa hivyo hawakuathiriwa na ufurushaji uliotokea Novemba 2019. Tatu kati ya familia zilizohama AGL, ziliishi upande wa Kedong wa Mlima Tatu huku moja ikihamia Kambi Turkana kwa muda. Kwa muujibu wa mzee wa kijiji cha Kambi Ya Gavana, mtu mmoja alidhibitishwa kuwa na makazi ya kudumu katika Kambi ya Gavana. Kwa kuzingatia maelezo ya hapo juu, jumla ya idadi ya familia katika Mlima Tatu ambazo zinastahiki kupata haki ya usuluhishi ni 14.

Tazama Jedwali 4-3 hapa chini:

**Jedwali4-3:MlimaTatu Haki ya Usuluhishi**

| Watu waliofukuzwa kutoka ardhi ya AGL katika eneo ya Mlima Tatu ya wa | Wanaume | Wanawake |
|---|---|---|
| **14** | 8 | 6 |
| **Jumla ya idadi ya watu wasiokuwa na haki ya kupata haki ya utatuzi kwa kufukuzwa** | | |
| **Hawakuwahi ishi Mlima Tatu.** | | |
| **4** | | |

**Sababu za kina za kustahiki katika Mlima Tatu.**

Shughuli ya Kuwapa makazi watu Mlima Tatu kabla ya Novemba 2019 ilienea katika ardhi ya Akiira na Ranch ya Kedong. Kwa mujibu wa taarifa alizopata mshauri kutoka kwa Mwenyekiti wa kikundi wa Mlima Tatu, ni jumla ya familia 48 zinazounda Mlima Tatu.

Makazi yaliathiriwa na ufurushwaji ufuatao:

- *Wakati fulani mnamo Agosti 2019, Kedong na Wakala wa Huduma za Misitu Nchini walipanga ufurushaji ulioathiri familia zote katika eneo ya Mlima Tatu. Myumba ziliripotiwa kuchomwa na Wakala wa Huduma za Misitu wkati huu wakufurushwa. Habari hii ilidhibitishwa kwa mshauri wa utawala wa serikali ya kitaifa, Tume ya Kitaifa ya Haki ya KIbinadami na, jamii za wenyeji katika jamii ya Kedong .Baada ya ufurushaji huu, baadhi ya familia zilihama kutoka ardhi ya Akiira na kuenda kukaa kwenye ardhi ya Kedong. Familia zingine zilihama kutoka Mlima Tatu na kuhamia Kambi Turkana. .*
- *Ufurushaji wa pili ulifanyika mnamo Novemba 2019 na uondowaji huu ulitekelezwa kwa amri na polisi kutokana na ombi la timu ya Usalama ya Kaunti Ndogo baada ya malalamiko ya AGL Kabla ya kufukuzwa huku, wenye nyumba upande wa Akiira wa Mlima Tatu walikuwa wanafahamu kwamba ufurushaji unaendelea Lorropil na hivyo, walihamisha mali zao kabla ya polisi kufika Mlima Tatu na kuteketeza nyumba hizo.*

***Upataji wa haki ya Usuluhishi kwa ukamilifu au sehemu yake tu.***

Kati ya familia 18, familia 3 zilizohama kutoka AGL ziliishi Kedong upande wa Mlima Tatu huku moja ikihamia upande wa Kambi Turkana kwa muda. Kwa mujibu wa mzee wa kijiji wa Kambi ya Gavana, mtu mmoja alidhibitishwa kuwa na makazi ya kudumu katika Kambi ya Gavana. Kwa kuzingatia yaliyo hapo, jumla ya idadi za familia katika Mlima Tatu ambazo zinastahiki na zinazostahili kupata haki ya urekebishaji ni 14. Fauka ya hayo,familia zote 14 zinastahiki kupata malipo kamili.

Jedwali lililo hapa chini linaonyesha vigezo vya kustahiki ambavyo vitatumiwa na AGL kuwajuzu jinsi utatuzi unafaa ufanyike.

**Jedwali4-4:Vigezo vya kustahiki na kielelezi cha kupata Haki.**

| Vigezo(sababu) vinavyochangia kustahiki | Ufafanuzi wa vigezo vya kustahiki (sababu) | Sababu # | Fidia ya kifedha | Fidia isiyokuwa ya kifedha | Msaada wa ziada | Fidia ya kifedha |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Jumla ya sababu hufafanua viwango vya kustahiki:*** | | | ***Familia zinazostahiki zina alama kati ya 15 na 17*** | | | ***Familia zinazostahiki zina alama 6 au chini ya hapo*** |
| ***1 .Tarehe ya mwisho kabla ya ufurushaji: Lorropil: Familia zilizofurushwa kutoka shamba la AGL walikuwa wakazi wa hapo kwa miaka kati ya 1-5. Mlima Tatu: Familia waliofurushwa kutoka shamba la AGL , tarehe ya mwisho ya kuishi hapo ndio tarehe ya kufukuzwa.*** | 1. Tarehe ya mwisho na kipindi cha kuishi (zaidi ya mwaka moja hadi mitano inaonyesha kudumu) na tarehe ya mwisho ikiwa Juni, 22 2019. Kwa Mlima Tatu hakuna utambulisho wa watu walioathiriwa ulifanywa na serikali na siku ya mwisho ya kuishi paleni Novemba 17, tarehe ya ufurushaji. | 1 | Hata kama haikuwezekana kudhibitisha upotevu mwingi wa mali iliyoharibiwa wakati wa kufurushwa, posho ya kubadilisha bidhaa za nyumbani ilitolewa kwa pesa taslimu.<br><br>Fidia ya pesa taslimu inaweza kutolewa kwa thamani sawa ya nyumba mbadala ikiwa Familia tayari imehama na kujenga nyumba nyingine au tayari inajenga upya nyumba iyo hiyo.<br>Posho ya mpito itatolewa.<br><br>Pesa zinapaswa kutolewa kwa njia iliyo salama zaidi (kwa kutumia benki kuwalipa waathiriwa walio na vitambulisho na pia AGL kuwezesha malipo kwa waathiriwa wasio na vitambulisho) na kiasi cha pesa kiwe siri.<br><br>Ambapo familia zimejumuisha mwanamume na mwenzi, wote wawili waliotajwa, wanapaswa kujumuishwa katika utaratibu wa malipo. | Fidia kwa vifaa kwa ajili ya nyumba zenye muundo wa kimsingi zilizoezekwa bati kama kuta na paa.<br><br>. | AGL kusaidia watu wanyonge na walio katika mazingira mgumu kupata fidia yao kwa kuwasaidia kufungua akaunti za benki na pia kuwalipa moja kwa moja wale ambao hawawezi kufungua akaunti.<br><br>Watu wowote wenye unyonge na wanaostahiki usaidizi wa kijamii watasaidiwa kupata usaidizi huo.<br><br>Posho ya usumbufu itatolewa ili kufidia hasara zisizoonekana ikiwa ni pamoja na ucheleweshwaji wa utekelezaji wa ulipaji fidia.<br><br>Familia zote zinapaswa kupata njia ya utatuzi wa malalamiko ambayo wanaweza kuamini. Njia hii inafaa iwe iliyoboreshwa, yenye usiri na isiyo ya gharama | Posho ya usumbufu itatolewa ili kufidia hasara zisizoonekana.<br><br>Pesa zinapaswa kutolewa kwa njia iliyo salama zaidi (kwa kutumia benki kuwalipa waathiriwa walio na vitambulisho na pia AGL kuwezesha malipo kwa PAP wasio na vitambulisho) na kiasi cha pesa kiwe siri.<br><br>Pale familia zinajumuisha mwanamume na mwenzi, wote wawili waliotajwa, wanapaswa kujumuishwa katika utaratibu wa malipo. |
| ***2 Nyumba zilizoharibiwa wakati wa ufurushaji ni nyumba mtindo wa Manyatta na myumba zenye paa tambarare ama zilizo na paa mara mbili.*** | 2. Kuwepo kwa aina za nyumba zilizotambuliwa kama miundo imara, zenye ushahidi wa kudumu kama vile sakafu iliyoinuliwa na kuta zilizoimarishwa dhidi ya hali ya anga. | 2 | | | | |
| ***3. Uwepo wa familia wakati wa ufurashaji.*** | 3. Kuwepo wakati wa ufurushaji mnamo Novemba 2019. | 3 | | | | |
| ***4. Uthibitisho wa ushahidiwa ukaliaji wa kihistoria wa eneo la uvamizi au kuwepo kwa eneo la makazi mahali pengine.*** | 4. Uthibitisho wa mashahidi (angalau mashahidi wawili) wa kuwepo kwenye makazi wakati wakati wa vipindi maalum ya kuishi pale na matukio ya kufurushwa pamoja na ushahidi halisi. | 4 | | | | |
| ***5. Familia hazina makazi mengine ya kudumu kando na eneo la ufurushwaji.*** | 5. Kuwepo kwa makazi ya kudumu pekee kwenye eneo la kufukuzwa. | 5 | | | | |

# 5. MBINU ZA USULUHISHAJI

Hatua za usuluhishaji zimeegemezwa katika kategoria tatu ambazo zimefafanuliwa katika sehemu ya 5.3 hapa chini na famila zao kulingana na athari zilizopatikana lakini zimeundwa kwa vipengele vifuatavyo.

### 5.1 Mpango wa Ushirikiano wa Wadau [1]

Mpango wa Ushirikiano wa Wadau unaotekeleza majukumu ulitayarishwa na AGL kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango kazi wa Usuluhishi. Mazungumzo yalianza na ufichuzi wa Mpango Kazi wa Mwisho wa Usuluhishi na yakaendelea wakati wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini. Kila shughuli ilikuwa na seti yake ya washikadau kutoka kwa waathiriwa waliojumuisha watu binafsi, wazee wa jamii, maafisa husika wa serikali (Naibu Kamishna wa Kaunti, Kamishna Msaidizi wa Kaunti, Chifu, Machifu Wasaidizi), mwakilishi wa Tume ya Haki za kibinadamu na usimamizi wa Kedong. Maoni kutoka kwa kila mmoja yaliandikwa na AGL kwa ufuatiliaji wa baadaye na marejeleo. Kumbukumbu ziliandikwa na kutiwa sahihi na wadau. Rejista ya wadau inayojumuisha wadau wakuu, wawasiliani, nyadhifa na majukumu kama yalivyofafanuliwa na Mpango wa Ushirikiano wa Wadau yalitayarishwa na AGL.

## 5.2 Utaratibu wa Utatuzi wa Malalamiko

Makala haya yalisahihishwa na kuidhinishwa mnamo mwezi wa Septemba 2022 wakati wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Usuluhishi. Vipeperushi vinavyohusu utaratibu wa malalamiko vilitayarishwa na kusambazwa wakazi wa ufichuzi wa Mpango Kazi wa Usuluhishi katika mikutano ya umma iliyofanyika katika vijiji vinne kama yalivyofafanuliwa katika sehemu ya 5.4.1. Wadau walihamasishwa kuhusu namna bora wanavyoweza kufikia AGL iwapo kuna masuala mbalimbali, manunguniko au malalamiko ndani ya mwezi mmoja na kuhusisha mikutano miwili ya umma kwa kila kijiji. Muda wa uandikishaji wa malalamishi mapya uliandikwa katika utaratibu ili kuepusha malalamishi zaidi baada ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Usuluhishi. Majadiliano zaidi juu ya malalamishi yamewasilishwa katika sehemu ya 5.5.

### 5.2.1 Muhtasari wa Utaratibu wa Malalamishi ya AGL

AGL inafuata utaratibu wa ngazi tatu za malalamiko, kama ilivyofupishwa katika sehemu zifuatazo:




### 5.2.2 Daraja la kwanza: Kiwango cha Jamii.

Kiwango cha Taratibu za Kusuluhisha Malalamiko katika cha ngazi ya jamii kinategemea miundo/mbinu ambazo zipo za usimamizi wa migogoro katika eneo la mradi. kinatoa jukwaa ambapo Jumuiya na wafanyakazi wa mradi husikiliza na kutatua malalamiko. Kiwango cha Taratibu cha Kusuluhisha Malalamiko inaongozwa na Kamati za Taratibu za Kusuluhisha Malalamiko (GRMC) ambazo zilianzishwa katika ngazi ambazo zinafaa. Kuanzisha Kamati za Taratibu za Kusuluhisha Malalamiko (GRMCs) kutafanywa rasmi kwa barua ya kazi na AGL katika ngazi mbalimbali.

Kamati imeundwa na wafuatao: AGL inawakilishwa na

- Meneja wa Nishati ya ESG Frontier
- Mtaalamu wa Kijamii wa AGL
- Maafisa wa Uhusiano wa Jamii wa AGL
- Chifu msaidizi wa eneo

- Chifu wa eneo
- Wawakilishi watano wa kamati za jumuiya (usawa wa kijinsia)

### 5.2.3 Daraja la pili: Kiwango cha Baina ya Jamii

Ngazi hii inashughulikia malalamiko ambayo yanahusisha malalamishi ya kijumla ambayo yanahusu vijiji vyote na inajumuisha wahusika kumi na mmoja kama ifuatavyo:

- Wawakilishi wawili kutoka Suswa
- Wawakilishi wawili kutoka RapLand
- Wawakilishi wawili kutoka Lorropil/ Kampi Turkana
- Wawakilishi wawili kutoka Mlima Tatu
- Chifu msaidizi wa eneo
- Chifu wa eneo
- Maafisa wa Uhusiano wa Jamii wa AGL
- Mtaalamu wa kijamii wa AGL

Kamati hii humchagua mwenyekiti wake (huku ikizingatia usawa wa kijinsia).

#### 5.2.4 Daraja la tatu: Kamati ya malalamiko ya kaunti ndogo.

Kamati za Taratibu za Kusuluhisha Malalamiko (GRMC), ya kiwango cha Kaunti ndogo imejengwa kwa mamlaka ya serikali ya kitaifa kama msimamizi wa maendeleo ya jamii na kuishi kwa utangamano kati ya wanajamii na miradi ya maendeleo. GRMC ya Kaunti Ndogo itashughulikia malalamiko yote yaliyopita kiwango kutoka kwa daraja la 1 na daraja la 2. Muundo huo utategemea aina ya malalamiko na, ikiwa inahusisha kijiji kimoja basi ni wajumbe wa kamati kutoka kijiji pekee ndio watakaoalikwa kwenye mchakato wa malalamiko ya daraja la 3.

Kamati imeundwa na wafuatao:

* AGL inawakilishwa na:
    * Meneja wa Nishati ya ESG Frontier
    * Mtalamu wa Masuala ya Jamii wa AGL
    * Maafisa wa Uhusiano wa Jamii wa AGL
    * Chifu msaidizi wa eneo wa AGL
* Wawakilishi watano wa kamati ya Lorropil
* Mwakilishi wa Shirika lisilokuwa la Serikali
* Wawakilishi wa Tume ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu ya Kenya, (KNHRC)
* Machifu wanaowakilisha maeneo ya Olkaria na Hellsgate
* Kamishna Msaidizi wa Kaunti kwa niaba ya Kamishna wa Kaunti.
* Wajumbe watano wa Kamati (wakiwakilishwa na Mwenyekiti na Msaidizi wake binafsi, Katibu, Mwakilishi wa Wanawake, Kiongozi wa Vijana na mwakilishi wa wazee).

Hiki ni kiwango cha mwisho cha mchakato wa utatuzi wa malalamiko ya AGL.

### 5.2.5 Kukata rufaa kwa Azimio.

Sheria za Kenya zinaruhusu mtu yeyote aliyenyimwa fursa ya kupata haki kupitia mfumo wa kiutawala na mahakama. Mswada wa Haki, Sura ya Nne ya Katiba, inadhamini idadi ya haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni, na hizi zinaonyesha viwango vya haki za binadamu vilivyoainishwa katika sheria za kimataifa za haki za binadamu. Kifungu cha 20 cha Katiba, kinaonyesha kwamba Mswada wa Haki unatumika kwa sheria zote na unathibiti vyombo vyote vya Serikali na watu wote (pamoja na makampuni ya biashara). Kifungu cha 22 hutoa ufikiaji wa suluhu kwa mtu yeyote anayedai kwamba amenyimwa haki au uhuru wa kimsingi kama ilivyo katika Mswada wa Haki, umekiukwa au kutishiwa. Iwapo mlalamishi bado hajaridhika na viwango vyovyote vilivyoundwa vya utaratibu wa malalamiko, ana haki ya kukata rufaa kwa mamlaka yoyote ya kisheria.

Mlalamishi ambaye hajaridhika na majibu yaliyopokelewa licha ya kuwa na fursa ya kuomba ufafanuzi zaidi au mrejesho, ana haki ya kufanya mawasiliano rasmi kwa Mwenyekiti GRMC akieleza sababu za kutoridhika. Mlalamikaji ambaye hakuridhika na majibu yaliyopokelewa kutoka kwa Mwenyekiti GRMC licha ya kupata fursa ya kuomba ufafanuzi zaidi au mrejesho, ana haki ya kufanya mawasiliano rasmi na GRM ya ngazi ya Kaunti ndogo akieleza sababu za kutoridhika.

*'Mlalamishi ambaye hajaridhika na matokeo baada ya kutatuliwa kwa malalamiko na mawasiliano kutoka kwa Mwenyekiti wa GRM ya Kaunti Ndogo anashauriwa kutafuta njia zingine za mahakama au za kiutawala, pamoja na Mahakama ya Mazingira na Ardhi (kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Kenya) au Utaratibu Huru wa Uwajibikaji wa wakopeshaji.'*

## 5.3 Uianishaji wa Walioathirika

Kwa mujibu wa sura ya 4, makundi ya waathiriwa yamechambuliwa na kutambuliwa kama ifuatavyo:

### 5.3.1 Kundi la 1: Jamii ya Lorropil – walioathirika ni 13.

Kategoria hii ilipoteza kila kitu wakati wa kufurushwa kwa hivyo ikazingatiwa kwa yafuatayo:

* *Posho ya mpito*
* *Posho ya usumbufu*
* *Vitu vya nyumbani*
* *Nyumba isiyo ya kudumu,yenye vyumba viwili na kuta za matope na iliyoezekwa paa ya mabati*

* ***Jumla ya kiasi cha Usuluhishi kwa aliyeathirika -(Shilingi 279,300***

### 5.3.2 Kundi la pili : Mlima Tatu – Watu walioathirika ni 14

Kategoria hii ilikuwa imeondoa vifaa vyao vya nyumbani kabla ya madai ya uchomaji wa nyumba kufanyika kwa hiyo yafuatayo yakazingatiwa:

* *Posho ya mpito*
* *Posho ya usumbufu*
* *Nyumba isiyo ya kudumu,yenye vyumba viwili na iliyoezekwa paa ya mabati*

* ***Jumla ya kiasi cha Usuluhishi kwa kila aliyeathirika - shilingi 265,700***

### 5.3.3 Kundi la tatu: Jamii ya Lorropil – walioathirika ni 31

*Kategoria hii inaunda idadi ya watu ambao walihamia katika ardhi ya Akiira kati ya Mei/Juni 2019 na tayari wana miundo ya kudumu kwingineko. Kategoria hii itapokea posho ya usumbufu.* ***Kategoria hii ilipokea tu posho ya usumbufu ya shilingi 55,000 kwa kila mwaathiriwa***

## 5.4 Mchakato wa utatuzi wa 2022

Mkutano wa kufichua mradi wa viongozi ulifanyika katika Hoteli ya Montana, Naivasha mnamo tarehe 8 Septemba 2022. Miongoni mwa viongozi waliohudhuria mkutano huo ni mwakilishi kutoka afisi ya DCC Naivasha, Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira ya Kenya**,** Mashirika ya Kiraia na mzee mmoja kutoka kila kijiji kati ya vijiji vinne vilivyo karibu na eneo la mradi la ambavyo ni Mlima Tatu, Lorropil, Suswa na Rapland.

Wadau walielezewa matokeo kutoka kwa mshauri wa kujitegemea na kusasishwa kuhusu Taratibu za Kusuluhisha Malalamiko za AGL . Maoni kutoka kwa mkutano pia yamejumuishwa katika ripoti hii.

### 5.4.1 Ushirikishi wa Jamii

Mikutano minne ya kutoa taarifa kwa jamii ilifanyika tarehe tofauti baada ya viongozi kukutana katika vijiji vifuatavyo:

* *Mkutano wa jamii ya Milima Tatu – Septemba 13, 2022*
* *Mkutano wa Jamii ya Lorropil – Septemba 15, 2022*
* *Mkutano wa jamii ya Rapland – Septemba 20, 2022*
* *Mkutano wa Jamii ya Suswa – Septemba 29, 2022*

Malengo makuu ya mikutano ya kijamii ilikuwa ni kuweka wazi ripoti ya Mshauri wa Mpango wa Urekebishaji ( rejelea 0131-1803) na Taratibu mpya za Kusuluhisha Malalamiko za AGL.

AGL pia ilichukua fursa hiyo ya kuwatambulisha Mlima Tatu na Kambi Turkana kama wadau ambao wametambulika wa mradi kuanzia wakati huo na hadi siku za usoni.

***Mkutano wa jamii ya Milima Tatu – Septemba 13, 2022***

Majina ya watu walioathirika na mradi, yalisomwa kwa jamii, na karibu yote yalifahamika na wanajamii. Hata hivyo, idadi kubwa ya wakaazi walihisi kuwa wameachwa nje. Walishauriwa kuandikisha malalamishi yao na AGL kwa kuzingatia utaratibu mpya wa kusuluhisha malalamiko.

***Mkutano wa jumuiya ya Lorropil – Septemba 15, 2022***

Jamii ilitambua majina mengi yaliyosomwa chini ya kategoria ya kwanza lakini ikakataa yale yaliyo chini ya kategoria ya tatu. Malalamishi yao yalibainika wazi na AGL ikawajulisha wale ambao hawakuridhika kuwasilisha malalamishi yao.

***Mkutano wa jamii ya Rapland - Septemba 20 2022 na mkutano wa jamii ya Suswa – Septemba 29, 2022***

Majina ya wote walioathirika katika orodha ya usuluhishi ni watu ambao walitoka eneo la Mlima Tatu na Lorropil. Mikutano ya jumuiya iliyofanyika Rapland na Suswa ilikuwa kwa ajili ya kubadilishana mawazo na kutoa maoni. Jumuiya hizi mbili zilifurahia hatua ya kuzima malalamishi ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu na ambayo yalitokana na kufukuzwa ambako walihisi kulisababisha mradi huo kudorora. Waliahidi msaada kwa mradi huo kwa matumaini kwamba uchimbaji utaanza tena, na jamii itafurahia manufaa yanayohusiana na mradi huo.

### 5.4.2 Ushirikishi wa watu binafsi walioathirika na mradi.

Baada ya mazungumzo yenye mafanikio na washikadau wakuu, walioathirika walifikiwa na kufahamishwa kuhusu haki zao mahususi. Fomu zilitiwa sahihi na kila mwathiriwa baada ya makubaliano. AGL ilishirikiana na benki ya Equity katika kutoa mafunzo ya usimamizi wa fedha na kufungua akaunti za benki kwa kila mwathiriwa. Baadhi ya waathiriwa hawakuwa na vitambulisho vya Taifa na hivyo hawakuweza kufungua akaunti za benki. AGL ilifungua akaunti ya pamoja inayosimamiwa na mtaalamu wake wa masuala ya kijamii ambapo fedha kwa wale ambao hawakuweza kufungua akaunti ziliwekwa.

Baada ya kufungua akaunti za benki kwa mafanikio, pesa zililipwa, na kila mwathiriwa alitia saini katika fomu ya kukubali malipo. Katika eneo la Mlima Tatu, waathiriwa 13 kati ya 14 waliostahiki chini ya kitengo cha 2 walilipwa. Mwathiriwa mmoja hajatambuliwa wala kufuafuatiliwa hadi leo.

Katika eneo la Lorropil, waathiriwa 10 kati 13 wa mradi, walishughulikiwa chini ya kategoria ya kwanza, na mwathiriwa mmoja alishughulikiwa chini ya kategoria ya 3. Waathiriwa wengine walikataa usuluhishi na kurekodi malalamishi.

### 5.4.3 Jumla ya gharama ya Usuluhishi 2022

Wakati wa awamu ya kwanza ya malipo ya watu walioathirika na mradi; watu 10 chini ya kategoria ya kwanza, watu 13 chini ya kategoria ya pili, na mtu mmoja chini ya kategoria ya tatu walishughulikiwa.

**Jedwali 5-1: Jumla ya gharama ya malipo ya usuluhishi ya 2022**

| Jina la kijiji | kategoria | Idadi ya walioathirika na mradi | Gharama (shilingi) | Gharama katika Dola ya Marekani @120/shilingi ya Kenya |
|---|---|---|---|---|
| **Lorropil** | 1 | 10 | 2,793,000 | 23,275.00 |
| **Mlima Tatu** | 2 | 13 | 3,454,100 | 28,784.17 |
| **Lorropil** | 3 | 1 | 55,000 | 458.3 |
| **JUMLA** | | **24** | **6,302,100** | **52,517** |

## 5.5 Malalamishi yaliyotokea kutokana na malipo ya usuluhishi.

Kufuatia ulipaji wa malipo ya usuluhishi katika awamu ya kwanza kama ionyeshwapo hapo juu, AGL ilipokea kirasmi malalamiko ya kwanza kutoka kwa mwenyekiti wa kamati ya Lorropil tarehe Oktoba 10, 2022 ikiwa wasiwasi zifuatazo:

* Walikosoa mbinu ya Mshauri kama isiyokubali mashauriano kwa kutowahusisha wazee wa Kijiji cha Lorropil wakati wa kuwatambua watu walioathirika na mradi.
* Taarifa fupi isio rasmi kwa walowezi katika ardhi ya Akiira.
* Kutokubaliana na orodha iliyowasilishwa ya majina na walidai kuwa baadhi ya majina ya watu katika orodha hawakuwahi kamwe kuishi katika Kijiji cha Lorropil.
* Data ya waathiriwa wa mradi, haikushirikiwa na jamii

Kwa kuwa jamii zilihamasishwa kuhusu Mchakato wa Taratibu za Kusuluhisha Malalamishi wa AGL, malalamishi zaidi yalipokelewa kama yalivyoelezwa kimhutasari katika jedwali hapa chini.

**Table 5-2: Malalamiko yaliyopokelewa kuhusu malipo ya usuluhishi.**

| TAREHE | NAMNA MALALAMISHI YALIVYOPOKELEWA | MALAMISHI YENYEWE | Hali ya malalamishi |
|---|---|---|---|
| **Oktoba 10, 2022** | Barua pepe ilitumwa kwa AGL | Ilipinga orodha ya waathirika wa mradi ya washauri na mbinu iliyotumika | Yamefungwa |
| **Oktoba 13, 2022** | Walioathirika na mradi walitembelea afisi ya AGL Naivasha na kurekodi malalamiko yao | Hawakukubaliana na kategoria iliyotumiwa na Mshauri ( kategoria ya tatu badala ya kwanza) | Yamefungwa |
| **Novemba 16, 2022** | Walioathirika na mradi, walitembelea afisi ya AGL Naivasha na kurekodi malalamiko yao | Wanadai kuachwa nje ya orodha ya Utatuzi na Mshauri | Yamefungwa |
| **Novemba 16, 2022** | Walioathirika na mradi, walitembelea afisi ya AGL Naivasha na kurekodi malalamiko yao | Hawakukubaliana na kategoria iliyowekwa na Mshauri( kategoria ya tatu badala ya kwanza) | Yamefungwa |
| **Januari 23,2023** | Walioathirika na mradi walitembelea afisi ya AGL Naivasha na kurekodi malalamishi yao | Wanadai kuachwa nje ya orodha ya usuluhishi na mshauri | Yamefungwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **7th Oktoba 23** | Mwathiriwa wa mradi, alituma barua pepe kwa AGL. | Maswali kuhusu Mwenyekiti, wakitaka kujua ni kwa nini aliyekuwa Katibu wa Marehemu mwenyekiti hakujumuishwa kwenye mikutano na kwa nini baadhi ya watu waliachwa. | AGL ilijibu barua hiyo kupitia barua iliyoandikwa tarehe Novemba 11, 2023 ambayo iliwasilishwa kwa mwathirika,siku iyo hiyo. |
| **Novemba 28,2023** | Yuleyule mwathiriwa wa mradi, alituma barua nyingine. | Kwa nini aliyekuwa katibu wa marehemu mwenye kiti hakujumuishwa kwa mkutano na kwa nini wanafamilia waliachwa nje. | Mkutano wa ana kwa ana ulifanyika tarehe 11, Januari 2024 kati ya AGL, mlalamishi na mshirika wake. Mlalamishi aliibua masuala yale yale kama yalivyoibuliwa hapo awali kuhusu uainishaji na mchakato wa ukusanyaji wa data ya mshauri. Masuala yote yaliyoibuliwa, yalishughulikiwa katika mkutano huo. Yako wazi kwa ukaguzi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Disemba 26,2023** | Mwathiriwa yuleyule wa mradi aliomba awe na mkutano rasmi na mtaalamu wa kijamii wa AGL kupitia kwa arafa. | Ili kujadiliana kuhusu barua pepe iliyotumwa tarehe 28, Novemba 2023 | Mkutano wa ana kwa ana ulifanyika tarehe 11, Januari 2024, kati ya AGL, mlalamishi na mshirika wake. Mlalamishi aliibua masuala yale yale kama yalivyoibuliwa hapo awali kuhusu uainishaji na mchakato wa ukusanyaji wa data wa mshauri. Masuala yote yaliyoibuliwa yalishughulikiwa katika mkutano huo. Yako wazi kwa ukaguzi |
| **Januari 15, 2024** | Mwathiriwa yuleyule wa mradi alituma barua pepe mnano Januari 15, 2024. | - Mwathiriwa wa mradi, aliainisha waathirika wa mradi, katika makundi ya ukabila.<br>- Waliibua masuala kuhusu uainishaji wa waathirika wa mradi.<br>- Jinsi gani au kwa nini waathirika wa mradi,kutoka kwa familia moja walilipwa chini ya kategoria tofauti<br>- Kwa nini mtu maalum alitolewa kutoka kwa orodha ya utatuzi | AGL ilijibu kupitia barua pepe mnamo tarehe 21, Februari 2024. Mlalamishi alithibitisha kwenye simu risiti ya barua, lakini bado hajajibu. Yako wazi kwa ukaguzi |

Kwa hiyo, malalamishi yakiwa yamerekodiwa, AGL ilianza ya Utaratibu wa Mchakato wa utatuzi wa Malalamishi uliohusisha mikutano ifuatayo:

### 5.5.1 Mkutano wa kwanza wa Daraja la kwanza uliofanyika tarehe 25, oktoba 2022 katika afisi ya AGL Naivasha.

Kamati ya malalamishi ya AGL ya Daraja la kwanza iliundwa na kuhudhuriwa na wafuatao:

* AGL iliwakilishwa kwa:
  Menaja wa Nishati Frontier ESG
  Mtaalamu wa Kijamii wa AGL
  Chifu msaidizi wa eneo wa AGL
* Chifu wa eneo wa AGL
* Wanachama watano wa kamati ya Lorropil ( wakiwakilishwa na mwenyekiti na msaidizi wake binafsi,katibu, mwakilishi wa wanawake, kiongozi wa vijana na mwakilishi wa wazee).

Kikao hiki kilitumika kutambua malalamishi yaliyowasilishwa na kamati ya Lorropil kupitia kwa Mwenyekiti wao wa Halmashauri. AGL iliwasilisha orodha ambayo ilitayarishwa na Mshauri wa kujitegemea. AGL pia ilitumia fursa hiyo kusasisha mkutano kuhusu waathiriwa ambao tayari walikuwa wameshughulikiwa

Kamati ya Lorropil ilidai kuwa na orodha tofauti ikilinganishwa na orodha ya Washauri. Chifu wa eneo la Hells' Gate pia aliarifu kamati hiyo kuhusu orodha ambayo ilikuwa imewasilishwa na wanachama wa Lorropil kama watu walioathiriwa na kufurushwa kwa afisi ya Chifu na Naibu Kamishna wa Kaunti katikati ya mwaka wa 2019 kabla ya kufurushwa. AGL pia ilikuwa na orodha ya majina ambayo yalirekodiwa kijijini kabla ya kufurushwa mnamo Agosti 2019. Hii ilifanya orodha hizo kufikia nne ( ya Mshauri, ya chifu wa kata la Olkaria, Orodha iliyowasilishwa kwa AGL mnamo 2019 na Lorropil 2022).

### 5.5.2 Mkutano wa pili wa Daraja la Kwanza, tarehe 8, Desemba 2022 katika afisi ya AGL, Naivasha.

Waliohudhuria mkutano ni wafuatao:

* AGL iliwakilishwa na:
  * Meneja wa Frontier Energy ESG
  * Mtaalamu wa Kijamii wa AGL
  * Maafisa wa Uhusiano ya Jamii wa AGL
* Chifu msaidizi wa eneo
* Chifu wa eneo
* Wanachama watano wa kamati ya Lorropil (wakiwakilishwa na mwenyekiti na msaidizi wake binafsi, katibu, mwakilishi wa wanawake, kiongozi wa vijana na mwakilishi wa wazee).

Ajenda kuu ya mkutano ilikuwa ni kulinganisho majina katika orodha nne. Jamii ya Lorropil ilijitenga na orodha tatu zilizotolewa lakini ilikubali orodha iliyokabidhiwa kwa AGL mnamo Novemba 2022.

Mwishoni mwa mkutano, hakukuwa na hitimisho, na hivyo ilikubaliwa kuwa mambo hayo yaongezewe katika daraja la GRM linalofuata ambalo lilihusisha wadau zaidi.

### 5.5.3 Mkutano wa kwanza wa Daraja la Tatu, tarehe 11, Mei 2023 katika shamba la Boffar, Naivasha.

Washiriki wa kamati ya malalamko ya Daraja la tatu ya AGL inaundwa na wafuatao:

* AGL inawakilishwa na:

  Meneja wa Nishati ya Frontier ESG
  Mtaalamu wa kijamii wa AGL
  Maafisa wa Uhusiano ya Jamii wa AGL

  Chifu msaidizi wa eneo wa AGL

* Wawakilishi watano wa kamati ya Lorropil
* Mwakilishi wa Shirika lisilo la Kiserikali
* Wakilishi wa Tume ya Kitaifa ya Haki za kibinadamu ya Kenya (KNHRC)
* Machifu wanaowakilisha kata za Olkaria and Hellsgate
* Kamishna Msaidizi wa Kaunti kwa niaba ya Kamishna wa Kaunti.
* Wanachama tano wa kamati ya Lorropil (wakiwakilishwa na mwenyekiti na msaidizi wake binafsi ,katibu, mwakilishi wa wanawake, kiongozi wa vijana na mwakilishi wa wazee).

Mkutano wa kwanza wa daraja la tatu ulihudhuriwa na washiriki wote wa kamiti. Kumbukumbu za mkutano wa daraja la kwanza zilisomwa, kuthibitishwa na kutiwa sahihi. Ajenda kuu ilikuwa uchambuzi linganishi wa orodha nne zilizowasilishwa na pande mbalimbali. Mkutano huo ulipendekeza yafuatayo.:

* Wale ambao walipatikana katika orodha tatu au nne walikubalika kwa malipo.
* Waathiriwa kumi wa mradi walioshirikishwa katika Kambi ya Gavana huko Mai Mahiu na kukariri kuwa hajawahi kuishi katika kijiji cha Lorropil lakini waliishi Mlima Tatu walitolewa katika orodha ya Lorropil.
* Waathiriwa wa mradi, 17 walipatikana kuwa hawifai kwani walipatikana kwenye orodha moja na kwa hivyo wakaondolewa.
* Majina 32 yalipitishwa katika mkutano huo na kuwekwa kwenye orodha ya usuluhishi.
* Kamati ilikubali kufanya uchunguzi zaidi wa waathiriwa wa mradi waliosalia.

### 5.5.4 Daraja la tatu, Mkutano wa Pili, uliofanyika tarehe 18 Mei, 2023 katika shamba la Boffar, Naivasha

Mkutano ulihudhuriwa na wanakamati wote isipokuwa mwenyekiti wa kamati ya Lorropil ambaye alikuwa mgonjwa wakati huo. Udhuru wake uliwasilishwa kwenye mkutano na Msaidizi wake wa kibinafsi na katibu. Ajenda kuu ilikuwa kujadili majina yaliyokuwa yakichunguzwa. Majina saba yalipitishwa kwa kauli moja na kuongezwa kati ya 32 yaliyokubaliwa katika mkutano uliopita. Majina 11 yalitupiliwa mbali huku majina manne yakitakiwa kuchunguzwa zaidi.

### 5.5.5 Daraja la tatu, mkutano wa tatu uliofanyika tarehe 15, Juni 2023 katika shamba la Boffar,Naivasha

Mkutano huo ulihudhuriwa na wanakamati wote na kaimu viongozi wapya kufuatia kifo cha mwenyekiti wa kamati ya Lorropil. Katibu wa kikundi alikaimu nafasi ya Mwenyekiti, na Kamati ikaleta mjumbe mpya. Kamishna Msaidizi wa Kaunti na Tume ya Kitaifa ya Haki za kibinadamu ya Kenya waliuliza kikundi cha Lorropil kwenda kufanya uchaguzi, ili mkutano unaofuata ufanyike na maafisa kamili.

Majadiliano kuhusu majina manne ambayo yalipaswa kuchunguzwa kwa mujibu wa mkutano uliyofanyika tarehe 18, Mei 2022 yaliwasilishwa kwa ajili ya kujadiliwa. Katika mkutano huo walikubali kuwaondoa wote kwani watatu kati yao hawakuwahi kuishi Lorropil huku mwingine jina la mwenzi wake lilikuwa kwenye orodha ya wanufaika. Baada ya majadiliano zaidi mahudhurio pia walikubali kwamba uainishaji wa walioathirika na mradi, ubaki kama ulivyoelekezwa na Mshauri. Kamati ya Lorropil iliomba wapewe muda wa kuipitia orodha hiyo na kufanya kategoria zao kwa kuwa hawakuridhishwa na kategoria ya mshauri. Ombi hili lilikubaliwa. Mkutano huu ulihitimishwa kwa kuthibitisha orodha ya waathirika wa mradi, wa Lorropil kuwa 38 na sio 44 kama ilivyopendekezwa hapo awali katika orodha ya washauri.

### 5.5.6 Daraja la tatu, mkutano wa nne uliofanyika tarehe 22, Septemba 2023 katika hoteli ya Montana, Naivasha.

Mkutano huo ulifanyika kufuatia uchaguzi wa viongozi wapya wa Kamati ya Lorropil uliofanyika tarehe 21, Agosti na kushuhudiwa na Chifu wa eneo hilo na msaidizi wake. Wanachama wengine wote wa kamati ya daraja la tatu walikuwepo kama ilivyofafanuliwa hapo juu na maafisa wapya wa Kamati ya Lorropil

Kikao kilijadili kuhusu uainishaji na kiasi kipya cha utatuzi

Mkutano huo ulifanya ukaguzi wa idadi ya watu katika makundi, kwa kuzingatia mashauri ya mikutano iliyofanyika tarehe Mei 15, 2023, Mei 18,2023 na 15 Juni, 2023. Kama ifuatavyo:

* Kategoria ya kwanza, kumi na tatu walisalia kulingana na pendekezo awali la Mshauri
* Kategoria ya tatu, idadi ya waathirika wa mradi, ilipunguzwa kutoka 31 hadi 25.

Kikao hicho pia kilifanya badaliko ya kiasi cha usuluhishaji kwa kuongeza kwa sababu ya mfumuko wa bei na usumbufu wa kusubiri kwa muda mrefu wa utelekezaji kama ifuatavyo:

* Kategoria ya kwanza iliongezeka kuoka shilingi 279,300 hadi shilingi 418,950
* Kategoria ya tatu iliongezeka kutoka shilingi 55,000 ( mwaka wa 2022) hadi shilingi 100,000

### 5.5.7 Daraja la tatu,Mkutano wa Ufuatiliaji, Oktoba 12, 2023, katika Hoteli ya Montana, Naivasha

Kwa kuwa mkutano huu ulikusudiwa tu kutia sahihi kumbukumbu za mkutano uliopita, mkutano ulihudhuriwa tu na wawakilishi wa AGL ambao walijumuisha Meneja wa Frontier ESG, Mtaalamu wa Kijamii wa AGL, Maafisa wa Uhusiano ya Jamii wa AGL na wajumbe wanne kati ya watano wa wanachama wa Kamati ya Lorropil. Kumbukumbu za mkutano uliopita zilisomwa na Mtaalamu wa Kijamii wa AGL na kuthibitishwa na AGL na wawakilishi wa Kamati ya Lorropil bila kufanyiwa marekebisho. Mkutano huo pia uliruhusu timu ya AGL kuanza mchakato wa malipo ya waathirika wa mradi walioidhinishwa.

## 5.6 Awamu ya pili ya malipo ya usuluhishaji,2023

Wakati wa awamu ya pili ya malipo, waathiriwa watatu wa mradi , chini ya kitengo cha kwanza na wengine 21 chini ya kategoria ya tatu, walishughulikiwa.

**Jedwali 5-3: Jumla ya gharama ya malipo ya usuluhishaji**

| Jina la kijiji | Kategoria | Idadi ya Waathiriwa | Gharama (shilingi) | Gharama katika dola ya Marekani @160/shilingi ya Kenya |
|---|---|---|---|---|
| **Lorropil** | 1 | 3 | 1,256,850 | 7,855.30 |
| **Lorropil** | 3 | 21 | 2,100,000.00 | 13,125.00 |
| **JUMLA** | | **24** | **3,356,850.00** | **20,980.30** |

## 5.7 Jumla ya waathiriwa wa mradi na gharama ya usuluhishaji hadi sasa.

AGL imewashughulikia waathiriwa wa mradi, katika kijiji cha Lorropil (kategoria 1 na 3) kama ifuatavyo:

* ***13 kati ya 13 ya walioathirika na mradi,*** *chini ya kategoria ya kwanza wameshughulikiwa*
* ***21 kati ya 25 ya walioathirika na mradi, chini ya kategoria ya tatu wamepata usuluhishi***
* ***3 kati ya 25 ya walioathirika na mradi, chini ya kategoria ya tatu wamehusishwa lakini hawajajitolea katika mchakato wa usuluhishi.***
* ***1 katii ya 25 ya waathirika wa mradi chini ya kategoria ya tatu wametafutwa bila mafanikio.***

AGL imefanya usuluhishi katika Kijiji cha Mlima Tatu (katagoria 2) kama ifuatavyo:

* ***Walioathirika na mradi ,13 kati ya 14 chini ya kategoria ya pili wamefanyiwa usuluhishi.***
* ***1 kati ya 14 ya waathirika, chini ya kategoria ya 2 wamefafutwa bila mafanikio.***

## 5.8 Jumla ya waathiriwa wa mradi, na malipo ya usuluhishi ambayo hayajalipwa hadi sasa.

Kulingana majadiliano sura ya 5.7 na malipo ya usuluhishi katika jedwali 5.4. Jedwali 5.4 hapa chini linaonyesha idadi ya waathiriwa na kiasi cha urekebishaji ambacho hakijalipwa. Hii inajumuisha waathiriwa, wote wawili ambao wamefuatiliwa bila mafanikio na wale ambao wamehusika lakini hawajajitolea katika mchakato wa usuluhishaji.

**Table 5-4: Jumla ya malipo ya utatuzi ambayo hayajalipwa hadi sasa.**

| Jina la kijiji | kategoria | Idadi ya waathiria | Gharama (shilingi) | Gharama katika USD@160/shilingi ya Kenya |
|---|---|---|---|---|
| **Mlima Tatu** | 2 | 1 | 265,700 | 1660.25 |
| **Lorropil** | 3 | 4 | 400,000 | 2500 |
| **JUMLA** | | **5** | **665,700** | **4160.25** |

AGL itaendelea na juhudi za usuluhishi hadi mwisho wa Machi 2024. Pesa za usuluhishi ambazo hazijalipwa zitaendelea kuwekwa hadi mwisho wa ukaguzi wa mchakato wa usuluhishaji wa AGL. AGL itahakikisha juhudi bora zaidi zinafanywa ili kupata makubaliano yaliyoandikwa na yaliyotiwa saini na waathiriwa wowote/wote waliosalia. Makubaliano haya ya maandishi ya kibinafsi yatatiwa saini na kushuhudiwa na uongozi na mamlaka za mitaa, kama ilivyokuwa kwa kesi ambazo tayari zimesuluhishwa.

## 5.9 Bajeti ya malalamishi yasiyotarajiwa ya usulihishi

AGL itatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya utatuzi wa malalamishi yasiyotarajiwa na bajeti hiyo itakuwepo hadi mwisho wa ukaguzi wa mchakato wa usuluhishi wa AGL. Hii inajumuisha malalamishi kutoka kwa Mlima Tatu na Lorropil.

# 6. UFUATILIAJI WA WAATHIRIWA, WAJIBU NA CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI

## 6.1 Maoni ya Ufuatiliaji wa Waathiriwa yatasasishwa Machi 2024

Ufuatiliaji ni muhimu na unapaswa kuwa sehemu ya utendaju mzuri wa usimamizi.Ufuatiliaji huu uliundwa kama shughuli ya ndani ya mradi,ili kutoa maoni ya mara kwa mara kuhusu maendeleo ya mradi,shida zinazokabili na kwa njia ufanisi ambao ulikuwa unatekelezwa. Kila mwezi, Mtaalamu wa Kijamii wa AGL na Maafisa wa Uhusiano wa Jamii hufanya mahojiano, uchunguzi, na ushirikiano na tawala za Kitaifa za Serikali za Mitaa ili kupata maendeleo ya waathiriwa

Waathiriwa wote ambao walilipwa mnamo 2022, walipewa muda wa miezi tano baada ya malipo ndio AGL ikafanya ufuatiliaji. Wengi wa waathiriwa walidhihirisha mabadiliko chanya katika maisha yao na walikuwa wameboresha viwango vyao vya maisha vya kijamii na kiuchumi. Jedwali 6.1 hapa chini ni ya Muhtasari wa ufuatiliaji na matokeo ya waathiriwa. Kwa wale waliolipwa mnamo 2023, mchakato wa ufuatiliaji na tathmini utaanza Januari 2024.

**Jedwali 6-1:Muhtasari wa Ufuatiliaji wa Waathiriwa**

| Kategoria | Idadi ya waathiriwa | Shughuli ya kiuchumi husika | Maoni |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | Walinunulia Familia ardhi . | Mwathiriwa mmoja alihama kutoka Kaunti ya Nakuru hadi Kaunti ya Turkana ambako familia yake pana iliishi. Alifanikiwa kununua kipande cha ardhi kutoka kwa pesa za usuluhishaji na kuishi.<br><br>Mwathiriwa mwingine alinunua ardhi huko Olesipukia katika kaunti ya Narok ambapo anaendeleza kilimo kama njia ya kujipatia riziki.<br><br>Waathiriwa hao wailili wa kike walifurahia sana kwamba wao sasa wanamiliki ardhi na kuishi na familia zao. |
| | 5 | Walinunua mifugo kwa ajili ya kufuga ili wapate mapato. | Waathiriwa walirudi katika ardhi ya mababu zao na kununua mifugo kwa faida za kiuchumi. |
| | 1 | Alinunua pikipiki na mifugo. | Kwa bahati mbaya muathiriwa huyu aliuza mifugo wote na pikipiki baada ya miezi miwili licha ya kupokea mawaidha kuhusu matumizi ya fedha kabla ya malipo |
| | 2 | Walitumia pesa za usuluhuhishaji kukamilisha ada za shule zinazodaiwa kwa watoto wao na pia kununua vitu vya nyumba. | Waathiriwa wa kitengo hiki walifurahia kuripoti jinsi walivyokamilisha kulipa masalio ya karo ya shule ya watoto wao kutokana na pesa za usuluhishaji. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | ***2*** | *Walinunua shamba, wakalipa karo na kuanzisha biashara.* | *Mwathiriwa mmoja chini ya kitengo cha tatu, alieka pamoja pesa zake na za dadake wawili na kununua nusu ekari ya ardhi katika eneo ya Ndabibi katika kaunti ya Nakuru*<br><br>*Sehemu ya fedha hizo ilitumika kukamilisha kulipia salio la karo*<br><br>*Mwathiriwa mwngine aliboresha nyumba yake na kuanzisha biashara ndogo ndogo katika eneo la Duka Moja ambayo itasaidia familia yake kiuchumi.*<br><br>*Mwathiriwa huyu alilipwa Januari, 2024 na amekodisha ekari kumi na tano za ardhi na kuanzisha ukulima.* |
| | ***1*** | *Kilimo* | *Mwathiriwa huyu alilipwa Januari, 2024 na amekodisha ekari kumi na tano za ardhi na kuanzisha ukulima.* |
| **2** | 5 | Walianzisha biashara ya familia. | Waathiriwa walianza kuuza mboga ,biashara halali ya kuuza makaa, na wengine wakaanzisha maduka rejareja. |
| | 3 | Walinunulia familia zao shamba. | Malipo yao yanewafanya kupata ardhi kwa ajili ya makazi. Kuna majibu chanya kutoka kwa hawa waathiriwa |
| | 2 | Walijenga nyumba za kukodisha kwa faida ya kiuchumi. | Walijenga nyumba za kukodisha katika mji wa Mai Mahiu ambapo walikuwa wamepewa ardhi na serikali katika kambi ya gavana. |
| | 2 | Walinunua pikipiki kwa faida ya kiuchumi. | Waliamua kuanzisha biashara ya kusafirisha abiria na bidhaa kwa kutumia pikipiki. |
| | 1 | Alikodisha ardhi kwa ajili ya kilimo kama shughuli ya kiuchumi kwa familia yake. | Kwa sasa anafanya ukulima ili kupata kipato kwa familia |
| **3** | 1 | Alikodisha ardhi kwa ajili ya kilimo kama shughuli ya kiuchumi kwa familia yake huko Nyahururu. | Alianzisha ukulima kama njia ya kujitafutia riziki. |
| | 20 | ***Walilipwa mnamo Novemba 2023 na Januari 2024.*** | ***Walifuatiliwa mnamoJanuari na Februari2024*** |
| | 11 | *Waliwekeza kwa kilimo* | *Walikodisha ardhi ili watumie kwa ukulima.* |
| | 5 | *Waliwekeza kwa elimu.* | *Walitumia pesa hizo kukamilisha karo ya shule ya watoto wao.* |
| | 5 | *Walitumia kwa matumizi ya nyumbani.* | *Walitumia pesa hizo kununua vyakula vya familia zao.* |

## 6. 2 Wajibu wa Utekelezaji

Mtalamu wa Kijamii wa AGL na Maafisa wa Uhusiano wa Jamii **(CLO)** wanasalia kuwa nguzo kuu za utekelezaji wa ripoti hadi kukamilishwa na kufungwa kwa malipo ya usuluhishi mwishoni mwa Septemba, 2024. Wanasaidiwa na Meneja wa ESG Nishati ya Frontier *na* ,kwa uangalizi wa jumla wa Wakurugenzi wa AGL kutoka Centum na Frontier. Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Frontier na Mshirika anayesimamia Mradi , wataongoza .

## 6.3 Changamoto za Utekelezaji

Zifuatazo ni changamoto kuu zilizojitokeza wakati wa mchakato wa utekelezaji:

* Ufuatiliaji na utafutaji wa waathirika wa mradi, - Baada ya kufurushwa baadhi ya watu walirudi kwenye makazi yao asili, na hii ilisababisha changamoto ya kuwatafuta kwa ajili ya usuluhishaji. Wafanyakazi wa AGL walilazimika kuendesha gari kwa umbali mrefu, Kilomita 100 kutoka eneo la mradi. AGL hata hivyo imeweza kufuatilia na kushirikisha waathiriwa 50 kati ya 52.
* ***Ukosefu wa simu –*** baadhi ya waathirika hawana simu na kuwafuatilia ilikuwa changamoto kubwa
* ***Ukosefu wa vitambulisho*** –baadhi ya waathirika wa mradi, hawakuwa na vitambulisho kwa hivyo hawakuweza kufungua akaunti za benki. Iliwalazimu AGL kutafuta namna waathiriwa hao wangelipwa kupitia akaunti ya Pamoja inayosimamiwa na kampuni.
* ***Udhibiti wa matarajio–*** Wengi wa waathirika, haswa wale walio chini ya katagoria ya tatu walitaka kuwa katika kategoria ya kwanza. Hili lilidhibitiwa kupitia mchakato wa utatuzi wa malalamiko.
* ***Viwango vya juu vya kutojua kusoma na kuandika-*** wengi wa waathirika wa mradi, hawafahamu kusoma wal kuandika. Hii ilileta changamoto kwa mchakato mzima wa usuluhishaji.
* ***Ufunguzi upya wa malalamish baada ya makubaliano ya GRM –*** Waathiriwa watatu wa mradi, wa Kijiji cha Lorropil (hasa familia moja) wamefungua tena malalamishi upya baada ya mchakato kupitia daraja zote za utaratibu wa usuluhishaji wa malalamiko na masuala kutatuliwa. AGL itaendelea kutia juhudi katika kuwashirikisha ili waweze kukubali usuluhisho uliokubaliwa.

## 6.4 Hitimisho

* Waathiriwa 47 kati ya 52 (90%) wanaostahiki walipata usuluhishi.
* Waathiriwa 3 kati ya 52 (5.8%) wameshirikishwa lakini hawajajitolea katika mchakato wa usuluhishi.
* Waathiriwa 2kati ya 52 (4%) wametafutwa lakini hawajapatikana.
* Juhudi bora zitafanywa kuoata makubaliano ya maandishi yaliotiwa sahihi juu ya suluhisho na baadhi au wote waliofurushwa.Makubaliano haya ya maandishi ya kibanfsi yatatiwa sahihi na kushuhudiwa na uongozi na mamlaka za mitaakulingana na kesi zote ambazo zimesuluhishwa.
* AGL itakuwa radhi kusuluhisha waathiriwa wowote waliosalia na ambao wanastahiki kupata usuluhishi lakini ambao bado makubaliano hayajapatikana hadi mwisho wa Septemba 2024.
* AGL itafanya ripoti ya mwisho ya ukaguzi wa kabla ya kufungwa ambao utafanywa na mtalamu huru wa kijamii na makazi kama sehemu moja wapo ya kufungwa kwa mchakato wa usuluhishi.Ripoti ya ukaguzi itafanya uhakiki wa kina wa matokeo ya utekelezaji wa RPF/RAP na Mpango Kazi wa Utatuzi dhidi ya malengo na mahitaji yaliyoainishwa katika mipango.
* Matokeo/ mapendekezo ya ukaguzi ya kabla ya kufungwa yatachukuliwa kwenye bodi na kufuatiliwa kama sehemu ya mkakati wa kufungwa.